




UKURASA 3

**TAKUKURU** yabaini rushwa ya ngono sekondari, msingi




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Februari 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581232

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Wahadhiri waibua hoja nyeti hakijinai

**WAWANYOOSHEA** kidole Polisi, TAKUKURU... *Endelea ukurasa 2*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia wakati akifunga Jukwaa la Uwekezaji na Biashara kati ya Tanzania na nchi za Umoja wa Ulaya (EU), Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## Bodaboda mbeba mkaa afa vurugu kwenye kizuizi

UKURASA 2

UKURASA WA 4

## MCHECHU ATEULIWA MSAJILI WA HAZINA



RAIS Samia Suluhu Hassan, amemteua Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba (NHC), Nehemia Mchechu, kuwa Msajili wa Hazina. Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, ilisema Mchechu...

UKURASA WA 4

## SILINDE AONYA WATUMISHI KUTEMBEA NA NYARAKA ZA SERIKALI MPAKA BAA

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amekemea tabia ya baadhi ya watumishi kwenda na nyaraka za serikali baa na nyumbani.
Waziri Silinde amesema hatua hiyo...

## Wawekezaji EU waona fursa, waja kuwekeza

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA, VIPERS VITA YA MAJIRANI** UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Mtaalam wa vifaa tiba wa Kituo cha Huduma za Utengamao kwa watu wenye ulemavu cha CCBRT Kituo cha Moshi, Neophita Lukiringi (kushoto), akionyesha namna bora ya kuchukua vipimo kwa ajili ya kutengeneza kitimwendo kwa mujibu wa viwango vya shirika la afya Duniani (WHO), kwa wajumbe wa bodi ya wakurugenzi wa hospitali ya CCBRT, walipokitembelea mkoani Kilimanjaro jana, kuelekea maadhimisho ya miaka 25 ya kituo hicho yanayofanyika leo. Wa (kushoto waliosimama) ni Rais wa Bodi hiyo, Dk. Willibrod Slaa na (kulia) ni Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Brenda Msangi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahadhiri waibua hoja nyeti hakijinai

**Na Restuta James**

WAHADHIRI wa vyuo vikuu wametaka watumishi wanaofanyakazi katika taasisi za hakijinai kuundiwa chombo cha kuwachunguza ili wanapokiuka maadili, wachukuliwe hatua za kisheria.

Wakizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana baada kutoa maoni kwenye Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Mifumo ya Haki Jinai, wahadhiri hao walisema kuundwa kwa chombo hicho kutaondoa upendeleo wapelelezi wanapokiuka maadili.

Aman Mwakolo, kutoka Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikatoliki Mbeya (CUCOM), alitoa mfano kuwa maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), wanapobainika kujihusisha na rushwa, wamekuwa wakipelekwa kwenye baraza la nidhamu jambo alilosema linaleta upendeleo.

"Kwa kuwa na wenyewe pia ni binadamu kuna uwezekano kabisa kwamba wakampendelea...ikitokea mtu wa TAKUKURU ametenda kosa la masuala ya rushwa wanashughulikia sana makosa ya kinidhamu na si kufikishwa mahakamani kama watuhumiwa wengine wa makosa ya rushwa," alisema.

Alisema wamependekeza mabadiliko ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 20 ili mtuhumiwa apewe vielelezo vya nyaraka kabla havijawasilishwa mahakamani kama inavyofanyika kwenye kesi ya madai.

Mhadhiri wa Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idd Mandi, alisema wamependekeza iundwe tume ya kusimamia maadili ya jeshi la polisi ambayo pamoja na mambo mengine, itapokea malalamiko ya wananchi na kuchukua hatua.

Alisema vyombo vya haki jinai viwezeshwe kivifaa na mafunzo kulingana na mahitaji ya sasa.

Alisema ushahidi wa kisayansi (Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali), ishuke hadi ngazi ya chini badala ya sampuli zote kuletwa Dar es Salaam jambo linalochelewesha kesi. Pia alipendekeza sheria ya dhamana irekebishwe na kuongeza makosa ya kudhaminiwa ili kupunguza msongamano magereza.

**ADHABU MBADALA**

Juzi jioni, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kaspar Mmuya, alipendekeza wafungwa wenye makosa madogo madogo wapewe zaidi adhabu mbadala badala ya kifungo ili kupunguza msongamano magerezani.

Mmuya alipendekeza kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Parole apewe mamlaka ya mwisho ya kuamua idadi ya wafungwa wa kutolewa na mfumo huo badala ya inavyoamuliwa sasa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Alisema wamependekeza kuwa mamlaka ya mwenyekiti yawe ya mwisho kwa sababu ni mteule wa Rais na wajumbe huchaguliwa na Waziri. Alipendekeza pia kuwapo kwa sheria itakayoelekeza aina za makosa yanayoruhusu adhabu mbadala ili kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani.

"Matamanio ya nchi sio kila aliyekosa akahukumiwe mahakamani bali lengo kama mfumo wa haki jinai ni kumfanya ajue kwamba amekosa, ajutie kosa lake na kuwa na wajibu wa kumrekebisha ili arudi kwenye jamii akiwa raia mwema na kujihusisha na shughuli zake za kijamii na kulinda amani ya nchi," alisema.

Mmuya pia amependekeza askari wa chini anapohukumiwa baada ya kutenda kosa, apewe nafasi ya kukata rufaa kwenye chombo huru ndani ya jeshi badala ya ilivyo sasa ambapo askari anakata rufaa kwenye sekretarieti ambayo wajumbe wake ni wakuu wa idara akiwamo ambaye anakuwa amemhukumu.

"Kwa muktadha huu utoaji wa haki unakuwa na mashaka kwa sababu yule anayemuhukumu mwanzo ndiye anamleta kwenye tume na yeye ni mjumbe ambaye anamsikiliza, hivyo kuna mazingira makubwa ya kukandamizwa kwa haki," alisema.

## Bodaboda mbeba mkaa afa vurugu kwenye kizuizi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

DEREVA wa pikipiki za kubeba mkaa, Abdallah Tenya, amefariki dunia wakati wa vurugu zilizotokea eneo la Vigwaza, Halmashauri ya Chalinze kwenye kizuizi cha Maliasili.

Inadaiwa kuwa vurugu hizo zilikuwa kati ya wafanyabiashara wa mkaa wanaotumia bodaboda na walinzi wa kizuizi kutokana na mmoja wao kukamatwa akitakiwa kulipa ushuru wa Sh. 50,000, kitendo ambacho hakuridhika nacho.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo, mmoja wa wafanyabiashara hao wa bodaboda alikamatwa na mlinzi wa halmashauri aliyekuwa kwenye kizuizi hicho, akitakiwa kulipa ushuru wa Sh. 50,000.

Kamanda Lutumo alisema mfanyabiashara huyo wa mkaa aligoma kulipa fedha hizo kisha akawapigia wenzake ambao walifika kwa wingi kwenye kizuizi hicho ili wakomboe bodaboda iliyokamatwa.

"Wakiwa na silaha za jadi, walivamia kizuizi hicho ili wachukue bodaboda iliyokamatwa na baadaye walitaka tena kumpokonya silaha mlinzi," alidai Kamanda Lutumo.

Aliendelea kusimulia kuwa watu hao walianza kumfanyia vurugu mlinzi huyo wa halmashauri wakiwa na silaha zao za jadi huku wakisema silaha anayotumia mlinzi huyo haifanyi kazi.

"Walitaka kumpokonya silaha mlinzi, sasa na yeye katika harakati za kujihami, alifyatua risasi ambayo ilimkuta mmoja wao ambaye ni Abdallah Tenya, mkazi wa Miswe ambaye alijeruhiwa na baadaye kupoteza maisha," alisema.

Kamanda Lutumo alibainisha kuwa mwili wa marehemu tayari umekabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inatamka katika ibara ya 14 kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inampa rukhsa askari kutumia silaha pale anapokuwa kwenye mazingira yanayohatarisha usalama wake, hivyo kulazimika kujihami.



Wafanyakazi wa kampuni ya usafi wakizoa takataka bila kuvaa vifaa vya kujikinga kama glovu katika eneo la Goba, Dar es Salaam mapema wiki hii, kitendo ambacho ni hatari kwa afya.
**PICHA: SABATO KASIKA**

# TAKUKURU yabaini rushwa ngono sekondari, msingi

**Na Christina Mwakagale**

MAENEO ya vyuo vikuu, shule za msingi na sekondari yamewekwa katika kipaumbele hivi sasa kupatiwa elimu ya kukabiliana na rushwa ya ngono kutokana na kukithiri kwa aina hiyo ya rushwa kwenye maeneo hayo.

Miongoni mwa maeneo ambayo yalibainika kuwapo kwa rushwa hiyo na kufanyika utafiti na kampeni kuanza, ni Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa kutoka Taasisi ya Kuzui na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Sabina Seja, akizungumza jana Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya miaka 15 ya Mfuko wa Udhamini wa Wanawake Tanzania (WFT-T), alisema taasisi hiyo imejikita kutoa elimu vyuoni kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Alisema kwamba tangu TAKUKURU ianze kufanya kazi na wadau tofauti, ukiwamo mfuko huo, kwa lengo la kuongeza haki kwa wanawake, kwa kipindi cha miaka mitano, walibaini rushwa ya ngono ndio huripotiwa zaidi maeneo ya vyuoni.

"Tulitia saini mkataba wa makubaliano kufanya kazi pamoja TAKUKURU na WFT-T. Tumefanya kazi nao kwa miaka mitano, kwenye mitandao ya kijamii rushwa hii huripotiwa matukio kadhaa ya ngono na utafiti uliofanyika, ulibaini hilo.

"Sasa tumejikita katika kutoa elimu kwa sababu namna ya waliokumbwa na matukio hayo kuyaripoti bado ni changamoto, angalau sasa utakuta kuna mijadala kama hiyo, ila mtu binafsi kuripoti ni ngumu," alisema Sabina na kuongeza:

"UDOM na UDSM, tulibaini kuna rushwa ya ngono na tukahamasisha namna ya kuepuka na vyuo vyenyewe vimeanza kutekeleza, kuzuia rushwa ya ngono. Tuliona si lazima kuwataja majina waliohusika ila tujikite katika kuelimisha."

Alisema taasisi hiyo inafanya kazi na wadau tofauti ili kupinga rushwa ya ngono maeneo tofauti mbali na vyuoni, ikiwamo mahali pa kazi na kwenye shule za msingi na sekondari, wakiwalenga zaidi walimu.

Mkurugenzi Mkuu wa WFT-T, Rose Marandu alisema mfuko huo ulioanzishwa mwaka 2008 kwa lengo la kuwawezesha wanawake katika kusaidia harakati za kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kijamii, ukitoa ruzuku kwa asilimia 60 kwa mwaka kwenye mashirika yaliyojikita kwa shughuli za pembezoni mwa nchi.

"Asilimia 60 tulitoa kwa maeneo ya pembezoni na asilimia 40 ya ruzuku zilitolewa ngazi ya taifa, kujenga mtandao unaoingiliana kisekta kama vile afya, elimu, uchumi. Lengo la maadhimisho haya ni kutafakari mafanikio, kujenga uelewa, kubaini changamoto na mbinu za kusonga mbele.

"Ingawa bado kuna vikwazo kwenye Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 pamoja na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, zinakinzana, upande huu inasema mtoto aolewe kwa ridhaa, wakati huo huo ni mtoto," alisema Rose.

Mgeni rasmi kwenye maadhiisho hayo, Mwenyekiti wa Mwenza wa Mfuko wa Equality Fund, Theo Sowa alisema Afrika bado ina changamoto na kwamba kuanzishwa kwa mfuko huo kumesaidia ndoto za wanawake wengi kuishi.

"Kabla ya waanzilishi wa WFT-T walibaini Kuna changamoto ya kifedha kwa wanawake, wakaja na wazo hili. Na ndoto yao ikatimia. Huu ni mafano bora lakini ikumbukwe Beijing ilibadili mtazamo kuhusu haki za wanawake duniani.

"Sherehe ya miaka 15 ya WFT-T ni muhimu kutokana na kazi, ndoto iliyofanikiwa. Umuhimu wa taasisi kama hii si fedha tu, lakini kuleta mapinduzi. Sehemu kubwa ya dunia hawajatambua kama kuwajumuisha wanawake kwenye shughuli tofauti, kuwa na sauti zao, huleta mabadiliko," alisema.

Kulingana na marekebisho ya kisheria ya mwaka 2016, Sheria ya Uhujumu Uchumi ya Mwaka 1984 na marejeo yake ya Mwaka 2002, ilifanyiwa mabadiliko na kufanya rushwa ya ngono kuwa jinai ya uhujumu uchumi.

Mwaka 2019, Mwanasheria wa TAKUKURU, Imani Nitume alizungumza na Nipashe kuhusu rushwa ngono, akitafsiri Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Mwaka 2007 kwa kurejea kifungu cha 25 kinachoainisha kwa upana.

Alisema: "Mtu yeyote ambaye kwa kutumia nafasi yake au mamlaka yake katika kutekeleza majukumu yake, anadai au analazimisha upendeleo wa kingono au upendeleo mwingine wowote kama kigezo cha kutoa ajira, kupandisha cheo, kutoa haki au upendeleo wowote unaotambulika kisheria, atakuwa ametenda kosa."

Taasisi hiyo kupitia mwanasheria huyo ilisema hivi sasa rushwa ya ngono ni kosa la uhujumu uchumi na adhabu yake siyo faini tena, ila ni kifungo cha mpaka miaka 20 gerezani.

# Wawekezaji EU waona fursa, waja kuwekeza

**Na Romana Mallya**

JUMUIYA ya Umoja wa Ulaya (EU) imeipatia Tanzania ruzuku ya Euro milioni 23 (Sh. bilioni 56.798) kusaidia utekelezaji programu za uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara (blue print), huku baadhi ya wawekezaji wake wakionyesha nia ya kuja kuwekeza kwenye sekta tofauti.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam wakati Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi alipofunga Kongamano la Biashara Kati ya Tanzania na EU lililofanyika kwa siku mbili, likihudhuriwa na washiriki 800 wakiwamo wawekezaji 270 kutoka nchi 27 za jumuiya hiyo.

Katika kongamano hilo kulitiwa saini mikataba ambayo thamani yake ni zaidi ya Euro bilioni moja.

Akizungumza kwenye kongamano hilo jana, Rais Mwinyi alisema EU inaipatia Tanzania ruzuku ya Euro milioni 23 kwa lengo la kusaidia utekelezaji wa programu hiyo pamoja na kuboresha kazi ya udhibiti wa ubora inayofanywa na Shirika la Viwango (TBS).

Alisema TBS itahakikisha bidhaa zinazozalishwa nchini zinakidhi viwango vya ubora wa kimataifa na hivyo kurahisisha kuyafikia masoko ya kimataifa, likiwamo la EU.

"Itahakikisha kwamba bidhaa zetu tunazozalisha zinakidhi viwango vya ubora wa kimataifa na hivyo kurahisisha ufikiaji wa masoko ya kimataifa ikiwa ni pamoja na soko la EU," alisema.

Rais Mwinyi aliwaeleza wawekezaji hao kuwa fursa za uwekezaji ambazo zipo kwenye sekta za kilimo, uchumi wa bluu, nishati mbadala, viwanda, madini, mafuta na gesi, ujenzi, usafiri na usafirishaji na huduma za kifedha zinazopatikana Tanzania Bara na visiwani Zanzibar.

Alisema dira ya serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuboresha mazingira ya sekta ya biashara na uwekezaji pamoja na ushindani wa kibiashara ili kuiwezesha sekta hiyo kuchangamka na kuchangia kwa kasi kubwa maendeleo ya uchumi na jamii.

Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Manfredo Fanti alisema kupitia kongamano hilo wawekezaji wa EU waliofika Tanzania, baadhi wameonyesha nia ya kurejea mapema kwa ajili ya kuendeleza mazungumzo yanayohusu uwekezaji sekta mbalimbali.

Pia alibainisha mikataba iliyotiwa saini kwenye kongamano hilo na thamani yake inafikia zaidi ya Euro bilioni moja.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Habiba Hassan Omar alisema kupitia kongamano hilo, wamewaeleza wawekezaji hao vivutio vilivyoko visiwani Zanzibar na kuwakaribisha kuwekeza sekta tofauti baada ya kuboresha mazingira ya biashara.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah alisema yaliyoafikiwa kwenye mkutano huo ambayo ni pamoja na kutiwa saini kwa mikataba hiyo, watahakikisha yanatekelezwa kwa vitendo.

"Matarajio yetu ndani ya uwekezaji ule tutaongeza ulipaji wa kodi kwa sababu vyanzo vya kodi vitakuwa vimeongezeka, tunatarajia uwekezaji ule utahitaji Watanzania kuajiriwa sekta za uchumi, maana yake dhamira ya Rais kuleta ajira inakwenda kutekelezeka kwa vitendo," alisema.

Juzi, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango alifungua kongamano hilo na kushuhudia utiaji saini wa hati tatu ikiwamo ya Huduma ya Usafiri wa Anga iliyotiwa saini na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbalawa na Waziri wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Uchumi wa Ufaransa, Olivier Becht.

Dk. Mpango aliwataka wawekezaji hao kuja kuwekeza kwenye maeneo yanayoendana na mahitaji.

Alisema lengo ni kuiwezesha Tanzania kutimiza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 na kutoka uchumi wa kati wa chini hadi uchumi wa kati wa katikati.

Alitaja vipaumbele vya nchi kwenye uwekezaji ni katika sekta ya kilimo, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo, viwanda vya dawa na vifaa tiba, ujenzi, sayansi, teknolojia, maendeleo ya viwanda katika kizazi cha nne.

"Serikali imedhamiria kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara kwa kuendelea kurekebisha sheria.

"Kuboresha mifumo ya ulipaji kodi ikiwamo sera za ulipaji kodi kwa nchi kumi, kuimarisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA)," alisema.

Makamu wa Rais pia alisema wanalenga kuimarisha upatikanaji wa umeme, uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, Bandari kavu ya Kwala, ujenzi wa barabara na reli na uanzishaji wa Sheria ya Uwekezaji ya 2022 ikifuta ile ya 1997.

Kadhalika, alisema jukwaa hilo linapaswa kuwa chachu ya kuongeza uwekezaji wa Umoja wa Ulaya nchini na kuwa sehemu ya kujenga imani na uaminifu kwa pande zote mbili.

# Mchechu ateuliwa msajili wa Hazina

**Na Mary Geofrey**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemteua Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba (NHC), Nehemia Mchechu, kuwa Msajili wa Hazina.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, ilisema Mchechu anachukua nafasi ya Mgonya Benedicto, ambaye atapangiwa majukumu mengine.

Rais Samia pia amemteua Hamad Abdallah kuwa Mkurugenzi Mkuu wa NHC, kuchukua nafasi ya Mchechu. Awali, Abdallah alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Gimcoafrica Limited.

Mchechu aliteuliwa kuliongoza shirika hilo Machi Mosi, 2010 na kabla ya uteuzi huo alikuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa iliyokuwa Commercial Bank of Africa (CBA)

Oktoba 30, 2018 alitenguliwa na aliyekuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, na nafasi yake kushikwa na aliyekuwa Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Ardhi, Dk. Maulid Banyani, aliyeongoza shirika hilo kwa takribani miaka minne.

Machi 14, 2022, Rais Samia alitengua uteuzi wa Dk. Banyani na kumrejesha Mchechu kwenye nafasi hiyo kwa mara nyingine hadi jana alipomteua kuwa Msajili wa Hazina.

Sambamba na uteuzi huo, Rais Samia jana alimteua Mussa Mohamed Makame kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC). Kabla ya uteuzi huo Makame alikuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya shirika hilo na mshauri mwelekezi wa masuala ya mafuta na gesi.

Makame anachukua nafasi ya Dk. James Mataragio ambaye uteuzi wake umetenguliwa na atapangiwa majukumu mengine.



Dk. Mataragio amefanya kazi kwenye shirika hilo tangu mwaka 2014, alipoteuliwa na Rais wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete.

Dk. Mataragio aliwahi kutenguliwa kushika nafasi hiyo kwa saa chache, kabla ya kutangazwa kurejeshwa tena na Rais Samia Aprili 14, 2021.

Aprili 3, 2021, Rais Samia alitangaza kumteua Thobias Richard kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC kuchukua nafasi ya Dk. Mataragio na kesho yake alitangaza kutengua utenguzi huo na kumrudisha Dk. Mataragio.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kulia), akikagua na kusikiliza maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa mabanda yatakayotumika kufugia ng'ombe kwa wanafunzi wa Kituo Atamizi cha Mabuki, wilayani Misungwi, mkoani Mwanza juzi, kupitia programu ya Samia Ufugaji kwa Tija (SAUTI) mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Silinde aonya watumishi kutembea na nyaraka za serikali mpaka baa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amekemea tabia ya baadhi ya watumishi kwenda na nyaraka za serikali baa na nyumbani.

Waziri Silinde amesema hatua hiyo inasababisha kuvuja kwa siri za serikali.

Silinde aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha makatibu tawala na wakuu wa idara katika mamlaka za serikali za mitaa jijini hapa.

Alisema bado kuna tatizo la baadhi ya watumishi hawatunzi nyaraka za serikali kwenye maeneo wanayosimamia na wengine wanatembea na majalada ya siri yakiwa hayajafunikwa.

"Wengine wanakwenda na nyaraka za serikali nyumbani na wengine wanatoa taarifa kuhusu nyaraka au jambo fulani kwenye baa. Hali hii inasababisha usalama wa nyaraka za serikali kutozingatiwa na hivyo kuhatarisha ustawi wa taifa," alisema.

Aliagiza wakuu hao kudhibiti uvujaji wa siri za serikali katika zama hizi za utandawazi na mitandao ya kijamii ili kuongeza uadilifu katika utumishi wa umma.

"Siri ndio uhai wa serikali, siri za serikali zikitoka nje zinasababisha kudharaulika," alisema.

Kuhusu uendeshaji wa mashauri ya nidhamu kwa watumishi wa mamlaka za serikali za mitaa, Naibu Waziri huyo alibainisha kuwa baadhi yamekuwa hayahitimishwi kwa wakati na watumishi hawapati nafasi ya kujitetea ili haki itendeke. Aidha, alisema serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi katika kushughulikia masuala ya nidhamu za watumishi hususani kwa yale ambayo wakati wa kushughulikiwa hayakufuata taratibu za uendeshaji.

Akizungumzia usimamizi wa mfumo wa uhamisho kwa watumishi wa umma, Silinde alisema uzoefu umeonyesha kuna baadhi ya watumishi wanaohama kwa sababu mbalimbali lakini barua zao zinafichwa licha ya mamlaka kutoa kibali.

Kadhalika, alisema ofisi hiyo tayari imeanza kupima utendaji kazi wa wakuu wa idara wote na haitasita kuchukua hatua kwa yeyote mwenye utendaji usioridhisha.

Mkurugenzi wa Idara ya Serikali za Mitaa wa Ofisi hiyo, Angelista Kihaga, alisema maofisa hao wana jukumu la kuhakikisha watumishi wao wanatunza siri na kuepuka ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma.

# Wodi watoto njiti yang'oa ofisa TASAF

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratias Ndejembi, ameagiza kubadilishiwa majukumu Mratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Halmashauri ya Mji Njombe, Peter Magehema.

Ndejembi ametoa agizo hilo ,baada ya kubainika uzembe wa kucheleweshwa mradi wa jengo la watoto waliozaliwa na uzito pungufu (njiti) katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji Njombe iliyoko Kibena.

Alitoa agizo hilo jana mjini hapa baada ya kukagua na kubaini kuchelewa kwa mradi huo ambao alisema umesababishwa na uzembe wa waratibu wa TASAF.

"Huu ni uzembe. Ulikuwa unafanya kazi gani kabla hujawa mratibu wa TASAF? Basi wewe urudi kwenye kilimo, mkurugenzi tafuta mratibu mwingine wa TASAF. Waandikie TASAF makao makuu, huyu arudi kwenye majukumu yake ya kawaida. Hili limemshinda kwa sababu hizi ni huduma za wananchi. Unavyochelewesha kwa uzembe, uratibu wa TASAF haukufai. Tunataka waratibu ambao wataratibu na shughuli ambayo itakwenda," alisema.

"Sasa wewe mratibu unakaa mwaka hela imekuja Febuari, 2022 na ulijua Sh. milioni 93 haiwezi kumaliza hapa. Kuna Sh. milioni 93 ilishawahi kumaliza hii. Mratibu gani usiyejielewa, basi bwana mrudisheni kwenye kilimo tupeni mratibu mwingine ambaye anaweza kuratibu shughuli za TASAF," aliongeza.

Awali, Magehema alimweleza Naibu Waziri kwamba mradi huo umechelewa kwa sababu fundi alikuwa anadai malipo yote kabla ya kuanza mradi pamoja na mfumo kusumbua.

Kaimu Mganga Mfawidhiwa Hospitali ya Halmashauri ya Mji, Dk. Ayubu Mtulo, alisema kuchelewa kwa mradi huo kunafifisha jitihada za kuwahudumia watoto njiti kwa sababu kwa mwezi wanapokea watoto 32 wakati chumba kilichopo kina uwezo wa kuhifadhi chini ya watoto 10.

## AfDB yaridhishwa utekelezaji miradi umeme

**Na Zuena Msuya,** DODOMA

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) anayewakilisha Tanzania, Ronald Cafrine, amesema ameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususani ya nishati.

Aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya kutembelea kituo cha kupokea na kupoza umeme cha Zuzu mkoani Dodoma ambacho benki hiyo imeshiriki kuchangia ufadhili wa gharama zilizotumika katika ujenzi wa kituo hicho.

Katika ziara hiyo, Cafrine aliambatana na ujumbe wake pamoja na maofisa waandamizi kutoka Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Cafrine alisema lengo la ziara hiyo ni kukagua miradi ya umeme inayofadhiliwa na Benki hiyo ili kujionea utekelezaji wake na hatua iliyofikiwa kutokana na fedha zinazotolewa na benki hiyo.

Baada ya kuona hali halisi ya utekelezaji, alisema miradi hiyo imefikia hatua nzuri za utekelezaji wake. Pia aliahidi kuwa AfDB itaendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania katika kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo ya ujenzi, maji na nishati.

Aliipongeza Wizara ya Nishati na taasisi zilizo chini yake kwa usimamizi mzuri wa fedha zinazotolewa na benki hiyo katika kutekeleza miradi husika. Aliahidi kuendelea kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali katika kuwaletea maendeleo Watanzania.

Akizungumza kwa niaba ya Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Kaimu Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi Christopher Bitesigirwe, alisema Tanzania ni nchi inayoendelea kukua, inahitaji zaidi nishati ya umeme katika kuhakikisha uchumi wake unakua na kufikia kiwango kitachotakiwa duniani.

Alisema kuwa na umeme wa uhakika, wa kutosha na wa gharama nafuu itasaidia kutimiza malengo yaliyowekwa kwa ajili ya maendeeo ili kutimiza malengo iliyojiwekea ya nyanja mbalimbali.

Pia alisema AfDB imetoa mchango mkubwa katika miradi ya kuzalisha, kusambaza na kusafirisha umeme katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo miradi ya kufua umeme kwa kutumia maji ya Kakonko, Malagarasi na mradi wa kusafirisha umeme mkubwa wa msongo wa Kilovolti 400 kutoka Iringa - Dodoma - Shinyanga hadi Namanga.

Mradi mwingine ni wa kusafirisha umeme wa msongo wa Kilovolti 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi, na mradi wa msongo wa Kilovolti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma.

# Waziri ataka upimaji maeneo uwekezaji

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesisitiza maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za uwekezaji nchini kupangwa, kupimwa na kumilikishwa kwa lengo la kuepuka migogoro ya ardhi.

Dk. Mabula alisema hayo jana katika ofisi ndogo za wizara, jijini Dar es Salaam, wakati akipokea taarifa ya mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha viwanja eneo lenye ukubwa wa ekari 630 lililoko mkabala na mradi wa kuchakata gesi asilia-LNG la Mto Mkavu na Likong'o mkoani Lindi. Mradi huo unatekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Waziri Mabula alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anasisitiza kuwekeza ni muhimu, hivyo mamlaka husika zihakikishe zinapanga, kupima na kumilikisha maeneo ya uwekezaji ili kuwarahisishia wawekezaji.

Kuhusu mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha viwanja katika eneo la Mto Mkavu na Likong'o, Dk. Mabula pamoja na kupongeza, alitaka kuwapo uwazi wakati wa mchakato mzima wa kutangaza viwanja vya mradi sambamba na kuepuka mtu mmoja kuchukua viwanja vingi ambavyo baadaye atashindwa kuviendeleza kwa wakati. "Hatuzuii mtu kuchukua viwanja lakini si mtu achukue mtaa mzima halafu anashindwa kuviendeleza na eneo kubaki vichaka. Sitotaka kusikia jambo hilo katika kipindi changu cha uongozi hapa wizara ya ardhi," alisema.

Pia aliitaka Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kuharakisha mradi unaojumuisha maeneo yote muhimu kama vile hoteli, huduma za kijamii, viwanja vya mpira na gofu, maeneo ya kupumzikia, shule, huduma za afya na maeneo ya viwanda.

Kupitia mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha viwanja, Manispaa ya Lindi imelenga kupanga na kupima viwanja visivyopungua 3,000 kwa ajili ya matumizi mbalimbali yenye sura ya kiuwekezaji kutokana na mpango wa mipangomiji ulioanishwa na kukubalika kulingana na mpango wa matumizi.

Akiwasilisha mpango huo, Mpima wa Manispaa ya Lindi, Kisna Mgeni, alisema halmashauri kwa kuzingatia mpango wa mipangomiji inategemea eneo la mradi kuwa na wakazi 13,000 na kuzalisha takriban ajira 5,400 kutokana na huduma mbalimbali za viwanda, biashara, afya, usafirishaji na elimu kwenye eneo hilo.

Kwa mujibu wa Mgeni, mbali na eneo la mradi kuwa la serikali, kuna baadhi ya wananchi wamefanya maendelezo kwa kuweka makazi na shughuli za kilimo kwa kumiliki mazao ya kudumu.

Alisema kutokana na azma ya halmashauri kuhakikisha wananchi wote wenye makazi Mto Mkavu na Likong'o wanamiliki maeneo yao kisheria, tayari halmashauri imepokea maombi ya kurasimishiwa makazi wananchi wote, hivyo eneo la ekari 293 nje ya eneo la serikali limeongezeka na kufanya mradi kuwa na eneo lenye ukubwa wa ekari 923.5.

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ilipokea mkopo wa Sh. bilioni 1.5 kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha viwanja kwenye eneo la Mto mkavu na Likong'o.



Ofisa mauzo wa kampuni ya Mohamed Enterprises Ltd, Jilala Jitabo (wa pili kulia), akikabidhi nyaraka na pikipiki 67 kwa Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Cyprian Mselem, wilayani humo, mkoani Tanga jana, zilizotolewa na serikali kwa ajili ya maofisa kilimo ili kurahisisha kuwafikia wakulima. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Bil. 3.1/- kuwawezesha wasaidizi wa kisheria

**Na Frank Monyo**

SHIRIKA la Legal Services Facility (LSF) limetoa ruzuku yenye thamani ya Sh. bilioni 3.1 kwa wadau wake ambao ni mashirika nufaika ya wasaidizi wa kisheria.

Wadau wengine ni mashirika nufaika ya wasaidizi wa kisheria, mashirika simamizi kwenye kanda sita na mashirika yanayotekeleza miradi kwenye maeneo muhimu ya kijamii, hasa uchumi kwa ajili ya uwezeshaji kisheria kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, akizungumzia ruzuku hiyo juzi, alisema sehemu ya ruzuku hiyo imetolewa kwa mashirika sita yatakayosimamia mashirika 92 ya wasaidizi wa kisheria kwenye kanda sita nchini ili kuongeza ubora, uwezo na maendeleo ya kitaasisi katika kutoa huduma bora za msaada wa kisheria kwa mwaka 2023.

"Ruzuku yenye thamani ya Sh. bilioni 2.08 imetolewa moja kwa moja kwa mashirika 184 ya watoa huduma za msaada wa kisheria pamoja na wasaidizi wa kisheria nchi nzima, Tanzania Bara na Zanzibar kwenye kila ngazi ya mkoa na wilaya zote kwa ajili kukuza upatikanaji wa haki kwa wananchi kupitia utoaji wa huduma za msaada wa kisheria bure.

"Ruzuku inayotolewa kwa mashirika ya watoa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria inakwenda kuchochea pia utekelezaji mkakati wa kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria ya Mama Samia iliojikita kutoa msaada wa kisheria kwa wanawake na watoto kwa kutoa elimu katika jamii kuhusu haki za binadamu, kupambana na ukatili wa kijinsia, utatuzi wa migogoro ya ardhi, masuala ya mirathi, kuelimisha wananchi kuhusu mifumo ya sheria, utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala pamoja na kujenga uwezo miongoni mwa wadau wa sekta ya msaada ya kisheria nchini," alisema.

Aliongeza kuwa sehemu ya ruzuku hiyo imetolewa kwa Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organization (KWIECO) kwa ajili ya kutekeleza mradi kwenye eneo la utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ya usuluhishi (Altenative Dispute Resolution - ADR).

"Mfumo wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi umeainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Ibara ya 107A(1) (d) ambayo inasisitiza kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro.

"Kuwapo kwa mfumo huu wa utatuzi wa migogoro kutawawezesha wananchi hususani wanawake na watoto kupata haki zao kwa wakati katika ngazi ya awali ya utatuzi wa migogoro," alisema.

Alisema ruzuku nyingine imetolewa na LSF kwa mashirika matatu kwa ajili ya kutekeleza miradi katika maeneo maalum ya kiuchumi, yaani 'Thematic Areas' kwenye sekta ya kilimo, madini na uchumi wa bahari kwenye mikoa ya Manyara na Lindi kupitia taasisi tatu za Community Support Initiatives Tanzania (COSITA), Lindi Association of Non-Governmental Organizations (LANGO), na Civic Social Protection Foundation (CSP).

Alisisitiza kuwa LSF kwa kushirikiana na COSITA itawezesha wanawake kupata fursa zitokanazo na mazao ya kilimo pamoja na kilimo chenyewe kwa kuwajengea uwezo pamoja na kuondoa vikwazo vya kijamii katika masuala ya umiliki wa ardhi ili kuwawezesha kufanya kilimo chenye tija na kuongeza mnyororo wa thamani katika kilimo wilayani Babati.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vita Ligi Kuu Tanzania Bara yahamia mkiani

**RAUNDI** ya 24 ya Ligi Kuu Tanzania Bara imeanza tangu juzi na hiyo inaamanisha raundi hiyo itakapokamilika, kila timu inayoshiriki ligi hiyo itakuwa imebakiwa na mechi sita tu ili kumaliza msimu wa mwaka 2022/2023.

Mpaka sasa mabingwa watetezi, Yanga ya Dar es Salaam ambayo inafundishwa na Mtunisia, Nasreddine Nabi, ndio vinara na wamejiimarisha baada ya kufikisha pointi 62, pointi nane tofauti dhidi ya watani zao, Simba yenye pointi 54 walioko katika nafasi ya pili,baada kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Azam FC.

Kama ambavyo lolote linaweza kutokea katika mbio za kuwania ubingwa, kwa wale walioko juu endapo watavurunda na kuwapisha walioukuwa wanawakimbiza, huu ni wakati wa kila timu kucheza karata zake vizuri kwa malengo ya kuvuna matokeo chanya.

Kihesabu inaonekana Yanga anahitaji pointi 15 ili kujihakikishia ufalme wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa msimu wa pili mfululizo au pointi 12, endapo itamfunga Simba katika mechi ya marudiano itakayochezwa Aprili 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mbali na Simba kuendelea kujiimarisha kwenye mbio za ubingwa, inahitaji kukusanya alama nyingi zaidi ili kujihakikishia tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao, kwa sababu nafasi hizo mbili za juu ndio hutoa tiketi ya kuiwakilisha Tanzania kwenye michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu.

Pia Wekundu wa Msimbazi wanafahamu endapo watamaliza katika nafasi ya pili, watapata zawadi nono kutoka kwa Azam Media, ambao wana haki ya kuonyesha mubashara mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye televisheni.

Kutokana na kusuasua kwa Simba na Azam FC kwenye vita ya kumvua Yanga ubingwa, sasa hivi macho na masikio ya wadau wa soka nchini wameyaelekeza zaidi katika kufahamu ni timu zipi zitashuka daraja na zipi zitajinusuru na janga hilo gumu kwa makocha na wachezaji wa klabu husika.

Vita ya kushuka daraja inaonekana ni ngumu zaidi kwa sababu lolote linaweza kutokea katika timu nane zinazoshika mkia, na hii inatokana na tofauti ndogo ya pointi walizonazo na mechi nyingine kucheza wao kwa wao. Timu ambazo mpaka sasa ziko katika mstari mwekundu lakini zinaweza pia kujikwamua na janga hilo ni pamoja na Ruvu Shooting ya Pwani, Polisi Tanzania (Moshi, Kilimanjaro), Prisons (Mbeya), Coastal Union (Tanga), KMC FC (Dar es Salaam), Dodoma Jiji (Dodoma) na Mbeya City ya jijini Mbeya.

Timu zote zinazoshiriki ligi zinatakiwa kuendelea kupambana na kutokata tamaa kwa sababu itajiweka pia katika nafasi nzuri ya kufanya tathimini ya kikosi chake kuelekea msimu mpya, makocha watafahamu madhaifu wanayotakiwa kuyaboresha.


Mbali na timu, wachezaji nao wanatakiwa kutokata tamaa na kuendelea kucheza kwa juhudi kwa sababu kupitia mechi hizo za mwisho, wanaweza kujitangaza na hatimaye wakasajiliwa na timu nyingine licha ya klabu zao za sasa kumaliza msimu vibaya kama ilivyotokea kwa beki wa Simba, Shomary Kapombe, aliyetua kwa Wekundu wa Msimbazi huku timu yake ya Polisi Morogoro ikishuka daraja.

Katika kuhakikisha ligi hiyo inamalizika salama na kila timu ikavuna ambacho inastahili, huu ni wakati wa kuhakikisha umakini na utulivu wa kutafsiri sheria unafanyika kwa kiwango cha juu na si kupendelea upande wowote.

Tunawakumbusha waamuzi waliobakia na ambao kwa sasa wameaminiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutenda haki katika michezo iliyobakia ili hatimaye bingwa anayestahili apatikane sambamba na timu zitakazoshuka daraja na kuelekea Ligi Kuu ya Championship, ziwe zimeachana na ligi hiyo ya juu bila ya malalamiko.

Kutenda haki kutasaidia Tanzania kupata wawakilishi watakaokwenda kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, ambao ni imara na watakaolipa taifa heshima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Simba inatakiwa isukwe upya, wengi umri tatizo

**NAKUMBUKA** Simba ya mwaka 1976 ambayo ilitwaa ubingwa wa Tanzania Bara, na ikafanya hivyo kwa miaka mitano mfululizo hadi 1980.

Ni Simba iliyotikisa si Tanzania tu bali hata bara zima la Afrika. Ndiyo hiyo iliyofungwa nyumbani mabao 4-0 na Mufulira Wanderers FC ya Zambia katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mwaka 1979 na kwenda kupindua meza kwa kishindo kule Lusaka, ikashinda magoli 5-0 na kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Ilikuwa Simba ya kutisha ikiwa na wachezaji kama Athumani Mambosasa, Omary Mahadhi, Daudi Salum 'Bruce Lee', Mohamed Kajole 'Machela', Athumani Juma, Mohamed Bakari 'Tall', Abbas Kuka, Williy Mwaijibe, Nico Njohole, Abdallah Mwinyimkuu, Thuwein Ally, George Kulagwa, Adam Sabu, na wengineo wengi.

Ni kikosi kilichokaa kwa muda mrefu kiasi cha kuzoeleka, na hata ukimwamsha usingizini shabiki wa soka wa klabu hiyo akupangie, atapanga hivyo hivyo.

Hakuna marefu yasiyokuwa na ncha, mwaka 1981, dalili zilianza kuonekana kikosi hicho baada ya mafanikio makubwa kimeanza kuchoka. Kilifungwa bao 1-0 na Yanga, bao lililowekwa wavuni na Juma Mkambi 'General'. Ndiyo wakati ambao Yanga nao walikuwa wamejitafuta sana na kupata wachezaji vijana ambao wakaanza kunyanyasa na kutawala soka la nchi dhidi ya wachezaji walioonekana wamechoka wa Simba.

Yanga ikatwaa ubingwa, na kuanzia hapo viongozi wa Simba wakaanza safisha safisha ya wachezaji wote ambao wanaonekana wamecheza kwa muda mrefu na tayari umri umeanza kuwatupa mkono.

Hawakujali tena jina la mtu, mradi walichokuwa wakitaka ni kuitengeneza tena timu upya, wakahangaika huku na huko kukusanya wachezaji wengine vijana ambao nao wakaja kufanya makubwa baadaye.

Nimeanza kwa hicho kilichotokea miaka miaka ya nyuma, nikiilinganisha na Simba hii inayoonekana leo. Simba, baada ya kukosa ubingwa kwa miaka mitano mfululizo tangu msimu ilipotwaa mara ya mwisho msimu wa 2011/12 hadi 2016/17, msimu minne ikichukuliwa na Yanga na msimu mmoja Azam FC, ilijitengeneza na kusajili wachezaji mbalimbali kutoka mataifa ya nje wakiwamo Felix Sunzu kutoka Zambia, Emmanuel Okwi wa Uganda, John Bocco, Erasto Nyoni, Shomari Kapombe, na Aishi Manula kutoka Azam, Mohamed Hussein 'Zimbwe' Jr' kutoka Kagera Sugar na wengineo.

Wachezaji hao walianza kujitengenezea utawala si kwenye soka la Tanzania tu, bali hata nje ya mipaka. Waliiwezesha kutwaa ubingwa msimu wa 2017/18 hadi 2020/21 ambapo ulikwenda kwa Yanga.

Nadhani viongozi wa Simba kama wangekuwa na uwezo wa kunusa hatari ulikuwa ndiyo msimu wa kufanya usajili mkubwa kwa ajili ya kuchukua namba za hawa waliopo. Haikufanyika, badala yake ilionekana kama wanasajili wachezaji wa kwenda kukaa benchi na kuwategemea wale wale. Kengele ya hatari nyingine ilikuwa ni pale Simba ilipotolewa katika Ligi ya Mabingwa dhidi ya Jwaneng Galaxy, ikiangukia kwenye Kombe la Shirikisho. Nilidhania baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu Bara, viongozi wangetulia na kufanya usajili mkubwa, badala yake bado usajili wao ulionekana kwa asilimia 70 unawategemea wale wale waliokuwapo.

Hata walipokuwa wakicheza Kombe la Shirikisho na kufika hatua ya robo fainali, Simba haikuwa ina kiwango kile ambacho ilikuwa nacho ilipotinga mara mbili hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika ikiwa na kina Meddie Kagere, Luis Miquissone, Chris Mugalu, Rally Bwalya, Okwi na wengine.

Wengi wanamlaumu Kocha, Roberto Oliveira kuwa mfumo wake ni mbaya, lakini ukweli ni karibuni nusu nzima ya wachezaji wa Simba wamechoka. Baadhi umri umewatupa mkono, wengine wamecheza kwa miaka mingi mechi mfululizo na hawana hata wasaidizi, huku wengine wakionekana kabisa hawana viwango vya kuichezea timu kubwa kama ya Simba,

Wakati Yanga inaweza leo ikamchezeha Djuma Shaaban kulia na Joyce Lomalisa kushoto, kesho inaweza kuwachezesha Kibwana Shomari na David Brayson na wakacheza bila matatizo yoyote, kitu ambacho hakipo kwa Simba.

# Washindi zaidi wazoa zawadi Serengeti

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia promosheni ya bia ya Pilsner Lager, ijulikanayo kama 'Kapu la Wana', imekabidhi zawadi za pikipiki, televisheni na simu janja kwa washindi saba wa droo ya kwanza ya promosheni hiyo kutoka mikoa ya Arusha, Mwanza na Mbeya.

Kati ya washindi hao, watatu walijishindia televisheni, wengine watatu simu janja na mmoja alishinda pikipiki. Makabidhiano ya zawadi hizo yalifanyika Kanda ya Ziwa, Kaskazini na Kusini ambako promosheni hiyo inafanyika.

Akizungumza kwenye makabidhiano ya pikipiki kwa mmoja wa washindi wa promosheni hiyo, Meneja Masoko wa SBL Kanda ya Ziwa, Ronald Lyatuu, aliwataja walioshinda kuwa ni Agatha Mvwango (Mbeya), Eli Elias (Arusha) na Hassan Joel (Mwanza) ambao walijishindia simu janja na walioshinda televisheni kuwa ni Justine Mwaipaja (Mbeya), Neema Abdallah (Mwanza) na Selina Panga (Arusha). Mshindi wa zawadi ya pikipiki ni Neema Mathias kutoka Mwanza.

Lyatuu alisema promosheni hiyo ilianzishwa kwa dhumuni la kuwawezesha wanywaji wa bia hiyo ambao ni wachapa kazi kwa kuwapa zawadi mbalimbali baada ya kushiriki kwenye promosheni hiyo.

"Hii ni mara ya pili tunafanya promosheni hii na kupitia promosheni hii tunataka kuwapa wateja wetu nafasi ya kuboresha maisha yao kwa namna tofauti. Kwa mfano mshindi wa hii pikipiki anaweza kuamua kutumia pikipiki hii kumwongezea kipato au vyovyote atakavyoamua kulingana na mahitaji yake," alisema.

Alitoa wito kwa wanywaji wa bia hiyo katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kusini na Kaskazini kuendelea kushiriki kwenye promosheni hiyo na kuwa kwenye nafasi ya kujishindia zawadi mbalimbali kupitia promosheni hiyo itakayofanyika kwa muda wa wiki nane.

Mshindi wa pikipiki, Neema Mathias aliishukuru SBL na kuwapongeza kwa kuandaa promosheni ya 'Kapu la Wana' ambayo ni maalum kwa kuwawezesha Watanzania wanaotaka kuboresha maisha yao.

"Nimefurahi sana kuwa mshindi wa hii pikipiki, natarajia kuitumia inisaidie kujiongezea kipato, nawashukuru sana SBL kwa kutuletea promosheni hii kwani kupitia zawadi hii naamini naenda kubadilisha maisha yangu una familia yangu kiuchumi," alisema.

Kwa washindi wa Arusha, makabidhiano ya zawadi za simu janja na televisheni yalifanyikia eneo la Ngusero na wale wa Mbeya, makabidhiano yalifanyika eneo la Roma Kyela mjini.

# Tani milioni 107 mazao zaingiza bilioni 223/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** DODOMA

SOKO la Bidhaa Tanzania (TMX) limefanikisha kuuzwa tani 107,059.619 za mazao mbalimbali yenye thamani ya Sh. bilioni 223.26 kati ya mwaka 2018 na 2022.

Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 212.09 sawa na asilimia 95 zimelipwa kwa wakulima.

Ofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutoka TMX, Goodluck Luhanjo, akizungumza jana katika mafunzo kwa wanahabari wa mikoa ya Singida na Dodoma kuhusu kazi zinazofanywa na taasisi hiyo, alisema mazao yaliyouzwa katika kipindi hicho ni ufuta, choroko, korosho, dengu, kakao na kahawa.

Alisema TMX imefanya uhamasishaji na programu za mafunzo kwa wakulima, wanunuzi, wenye viwanda, fedha, watunga sera na wasimamizi na zaidi ya wadau 190,000 wamefikiwa kwenye mikoa 25 ya Tanzania katika kipindi hicho.

Luhanjo alisema juhudi zilizofanywa na TMX ni kuhakikisha mapato ya ziada kwa mkulima kwa kilo ya bidhaa zilizouzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania na kufanikisha wastani wa faida kwa kilo kwa wakulima kuwa Sh. 1,600.

Meneja Uzalishaji, Augustino Mbulumi, alisema TMX tangu imeanza kutekeleza majukumu yake imeweza kuleta uwazi wa bei za bidhaa na mwenendo wa soko, ugunduzi wa bei kwa ushindani, kupunguza gharama za kuuza na kununua na pia imeweza kutoa kinga ya bei.

Alisema mfumo wa kielektroniki unaendelea kuboreshwa kuongeza bidhaa zaidi kwa ajili ya mauzo na kwamba TMX kupitia msaada kutoka TMEA imeanza kuweka mabango ya kidijitali katika baadhi ya maeneo ya kimkakati kwa ajili ya usambazaji wa taarifa za bei na soko kwa wadau na umma.

Mbulumi alisema TMX limeleta faida kwa mkulima kwa kuimarisha bei kwenye soko na hivyo kupunguza hatari ya upotoshaji wa soko,uwezo wa kupata mazao mengi na yenye ubora kwa wakati mmoja na pia imesaidia biashara ya kimataifa kwa gharama nafuu.

Alisema pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kuna changamoto kadhaa zikiwamo kuwapo maghala machache yanayozingatia viwango vya kuhifadhi mazao hasa nafaka, vyama vya ushirika kuzoea kutumia 'sanduku la zabuni' na njia zisizo za kidijitali. Aliongeza kuwa katika kukabiliana na changamoto hizo, serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana Bodi ya Stakabadhi Ghalani, imeanza mipango ya kuwa na ghala kwa kila wilaya katika maeneo yote ya uzalishaji.

Pia alisema TMX imeendelea kushirikiana na Balozi mbalimbali ili kupanua wigo wa wanunuzi nje ya Tanzania na kuimarisha mawasiliano kati yake, Bodi ya Stakabadhi Ghalani, Vyama Vikuu vya Ushirika, Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS), wakulima na wadau wengine.

Nao washiriki wa mafunzo hayo walishauri TMX kupanua wigo wa utoaji elimu kwa wakulima ili waweze kupata soko la uhakika la mazao yao na hivyo kilimo kuwasaidia kuboresha uchumi wao.

Walisema kwa kuwa vyama vingi vya ushirika pamoja na AMCOS zina changamoto nyingi kwenye malipo kwa wakulima, walishauri TMX ichukue jukumu la kuwalipa wakulima malipo ya mauzo ya mazao yao ili wawe na uhakika wa kupata fedha kwa wakati tofauti na sasa wanavyocheleweshewa.



Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde (wanne kulia), akizindua kampeni ya kilimo ya "Kijanisha Maisha" ya Taasisi binafsi ya kusaidia Sekta ya Kilimo (PASS Trust), jijini Dar es Salaam jana. Kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, John Kaduma, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Pass Trust, Dk. Tausi Kida (kushoto kwake) na viongozi wengine. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania wapewa mchongo nafasi kusoma PhD ughaibuni

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wameshauriwa kuchangamkia Shahada za Uzamivu (PhD), zinazotolewa na vyuo vya nje kwa bei rahisi ili kuongeza idadi ya wataalamu na wahadhiri wa vyuo vikuu nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Vyuo Vikuu Nje ya Nchi (Global Education Link-(GEL), Abdulmalik Mollel, alisema hayo jana jijini Dar es salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alikuwa akizungumzia maonyesho ya vyuo vikuu vya Cyprus, Uingereza, Uturuki, Malasyia na India yanayoanza leo kwenye hoteli ya Serena, Dar es Salaam.

Mollel alisema kuna baadhi ya watu wanaogopa kusoma Shahada za Uzamivu wakidhani kwamba zinagharama kubwa wakati nje ya nchi mafunzo hayo hutolewa kwa bei rahisi.

"Nitoe wito kwa wanafunzi wanaohitaji kusoma PhD mara nyingi wanafikiri vyuo vikuu nje ya nchi ni ghali sana na tunapokuwa na watu wengi wenye elimu ya kiwango hicho watatusaidia sana kujenga nchi yetu kwenye elimu.

"Sasa kwa mfano hivi vyuo ambavyo nimeleta mfano vyuo vikuu vya India, Cyprus, Uturuki PhD ni Dola 1,000 za Marekani hapo naongelea shilingi milioni mbili mpaka milioni nne kwa mwaka kwa kiwango cha PhD ni nafuu sana kwa sababu kuna vyuo hapa ndani gharama zinaweza kufikia hadi Sh milioni nane," alisema Mollel.

Alisema mwanafunzi anaweza kupata fursa ya kusoma Shahada ya Uzamivu kwa Sh. milioni 2.3 mpaka milioni nne na kwamba gharama hiyo kwenye vyuo vikuu mashuhuri duniani ni fursa kubwa.

"Kwa kuwa vyuo hivyo sasa viko nchini, naona ni fursa ya sisi kuongeza idadi ya wahadhiri wanaotamani kusoma ngazi ya Uzamivu tusiogope gharama hizi za vyuo vya nje gharama zake ni ndogo na nafasi zipo," alisema Mollel.

Alisema leo na kesho vyuo hivyo vitakuwa na maonyesho makubwa ya elimu kuwapa fursa wanafunzi watanzania wenye mahitaji ya masomo kwenye nchi za nje.

Maonyesho hayo, alisema yatafanyika katika ukumbi wa Serena kuanzia asubuhi hadi jioni na kwamba Jumapili yatafanyika kwenye viwanja vya Mapinduzi Square, Zanzibar na baada ya maonyesho hayo, vitaendelea na udahili wa wanafunzi.

Alisema kuanzia keshokutwa vitakuwa vinadahili wanafunzi wanaotaka kusoma nje ya nchi katika ofisi za GEL jijini Dar es Salaam hadi mwezi ujao.

"Kuna vyuo vimepunguza ada za masomo ya udaktari wa tiba kutoka shilingi milioni 30 kwa mwaka hadi shilingi milioni 10 kwa mwaka hii tunaona ni fursa sana kwa watanzania kuchangamkia na watakaofika watapata udahili siku hiyo hiyo bure," alisema.

# Mkakati wa usalama kimataifa ni muhimu kwa usalama wa dunia

**Na Chen Mingjian**

SUALA la usalama linahusu ustawi wa watu wa nchi zote kwa sababu ya amani na maendeleo ya dunia, na mustakabali wa binadamu.

Hivi sasa, mabadiliko makubwa ambayo hayajatokea katika karne yanaibuka kwa kasi ya haraka na dunia imeingia katika kipindi kipya cha msukosuko, kama inavyoonyeshwa na athari kubwa ya janga hili, kuongezeka kwa mawazo ya kupunguza utandawazi, migogoro ya ndani, misukosuko ya mara kwa mara, na masuala ya usalama ya kimila na yasiyo ya kimila.

Mwanadamu anakabiliwa na changamoto zisizo na kifani na jumuiya ya kimataifa inakabiliwa na suala la nyakati, yaani "Ni aina gani ya dhana ya usalama ambayo dunia inahitaji na jinsi nchi zinaweza kufikia usalama wa pamoja".

Kujenga dunia salama ni shauku kubwa ya watu duniani kote na pia ni shughuli isiyoyumba ya China. China inafuata njia ya maendeleo ya amani na iko tayari kutoa hekima yake na mpango wake wa kukabiliana na tatizo la sasa la usalama na kutafuta usalama wa dunia nzima.

Aprili, 2022, Rais Xi Jinping wa China alipendekeza Mpango wa Usalama Duniani (GSI) kwa mara ya kwanza katika hotuba yake kwenye sherehe ya ufunguzi wa Mkutano wa Mwaka wa Baraza la Asia wa 2022 wa Boao na kuelezea kwa utaratibu msimamo na mapendekezo ya China ya kukuza usalama kwa nchi zote duniani na kulinda amani na utulivu wa dunia. Pia alihimiza umoja katika kukabiliana na hali ya kimataifa iliyorekebishwa kwa kina na mbinu ya kila upande kunufaika katika kukabiliana na changamoto ngumu na zilizofungamana za usalama.

Mpango wa usalama wa kimataifa ni faida nyingine muhimu ya kimataifa ya umma ambayo China inachangia kwa dunia, ikilenga kutoa mwelekeo mpya wa kuondoa sababu kuu za migogoro ya kimataifa na kujibu changamoto za usalama wa kimataifa, na kutafuta suluhisho la muda mrefu la amani duniani na ustawi wa pamoja.

Tangu mpango wa usalama duniani ulipopendekezwa, umepokewa kwa umakini wa kina na mwitikio chanya kutoka kwa jumuiya ya kimataifa. Kwa sasa, zaidi ya nchi 80 na mashirika ya kimataifa yamepongeza na kuunga mkono mpango huo.

Wakati wowote, China inapopendekeza mpango wa kimataifa, haikai na kujivuna bali hukaa kimya na haifikirii mambo yasiyo na maana. China si tu mwanzilishi wa mpango huu mkubwa bali pia mwanaharakati thabiti wa kukuza utekelezaji wake.

Ili kuimarisha zaidi uelewa wa jumuiya ya kimataifa kuhusu mpango wa usalama duniani na kujibu matarajio ya pande zote, Februari 21, mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Qin Gang, alitoa hotuba katika sherehe za ufunguzi wa Jukwaa la Lanting kuhusu Mpango wa Usalama Duniani: Pendekezo la China la Kutatua Changamoto za Usalama. Alitangaza kutolewa kwa Andiko Dhana la Mpango wa Usalama Duniani.

Kutolewa kwa Andiko Dhana la Mpango wa Usalama Duniani, kunaonyesha dhamira ya China ya kudumisha amani ya dunia na azimio lake thabiti la kulinda usalama wa kimataifa. Andiko Dhana la Mpango wa Usalama Duniani linafafanua zaidi dhana na kanuni za msingi za Mpango huu: Kuendelea kujitolea kwa maono ya usalama wa pamoja, wa kina, wa ushirika na endelevu; kuendelea kuheshimu uhuru na sheria za kimataifa zinazotoa haki kwa nchi zote kulinda mipaka yake.

Pia linasisitiza kuendelea na nia ya kutii madhumuni na kanuni za Mkataba wa Umoja wa Mataifa; kuendelea kushughulikia maswala halali ya kiusalama ya nchi zote kwa umakini; kuendelea na nia ya kusuluhisha kwa amani tofauti na mizozo kati ya nchi kupitia mazungumzo na mashauriano; kuendelea kujitolea kudumisha usalama katika maeneo ya mila na yasiyo ya mila. Ahadi hizi sita zimeunganishwa na kuimarisha pande zote, na ni msingi wa kuunganisha tofauti.

Andiko Dhana la Mpango wa Usalama Duniani linafafanua zaidi maelekezo 20 muhimu ya ushirikiano kwa kuorodhesha maelekezo muhimu 20 kuhusu yaliyo mashuhuri zaidi ya dharura ya usalama ya jumuiya ya kimataifa kwa sasa, na ina mwelekeo wazi wa kushughulikia masuala kwa vitendo.

Kwa muhtasari, ni kuunga mkono kwa uthabiti jukumu la msingi la Umoja wa Mataifa katika usimamizi wa usalama; kujitahidi kukuza uratibu na mwingiliano mzuri kati ya mamlaka kuu; kukuza mazungumzo kikamilifu ili kutatua masuala muhimu kwa njia ya amani; kujibu kwa ufanisi changamoto za usalama za mila na zisizo za mila; na kuendelea kuimarisha mfumo wa utawala wa usalama wa kimataifa na kujenga uwezo.


China inatetea kwamba pande zote zinaendeleza kikamilifu ujumuishaji wa dhana na maslahi ya usalama katika nyanja zinazojumuisha, sio tu hizi 20, na kufanya kazi na China ili kusaidiana na kuimarishana na kukuza kwa pamoja amani na utulivu duniani.



Andiko Dhana la Mpango wa Usalama Duniani linapendekeza zaidi majukwaa na mbinu za ushirikiano zinazofaa. Andiko hilo limeorodhesha majukwaa matano ya ushirikiano na mbinu za kuunga mkono na kukuza utekelezaji wa Mpango huo, kwa matumaini ya kuingiza msukumo mpya na uhai katika majukwaa na mbinu zilizopo za ushirikiano katika uwanja wa usalama wa kimataifa.

Unakaribisha na kuhimiza majukwaa na mbinu mpya za ushirikiano ili kutoa chaguo zaidi kwa jumuiya ya kimataifa, na kufikia kwa pamoja katika misingi ya mazungumzo yaliyopo ya usalama na majukwaa ya ushirikiano.

Bila amani na usalama barani Afrika, hakutakuwa na utulivu na ustawi duniani. China ikiwa ni nchi kubwa zaidi inayoendelea duniani, imegawana shida na raha na idadi kubwa ya nchi za Afrika na ni mshiriki mwenye kujenga na mchangiaji mahiri katika masuala ya amani na usalama barani Afrika.




Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Qin Gang, akihutubia Jukwaa la Lanting. **PICHA:MTANDAO.**

China imependekeza na kuhimiza utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Ushirikiano wa Amani na Usalama kati ya China na Afrika ili kutoa misaada mbalimbali kwa juhudi za kulinda amani na utulivu wa Afrika. China pia imeshiriki kikamilifu katika operesheni za ulinzi wa amani za Umoja wa Mataifa huku karibu wanajeshi 2,000 wa China wakiwa kazini kwa sasa barani Afrika.

Aidha, China imekuwa ikijihusisha ipasavyo katika upatanishi wa masuala muhimu barani Afrika, na kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa katika matukio mbalimbali kuzingatia zaidi na kutoa msaada mkubwa kwa juhudi za Afrika katika kutatua masuala ya amani na usalama.

China pia imeshiriki kikamilifu katika operesheni za ulinzi wa amani za Umoja wa Mataifa huku karibu wanajeshi 2,000 wa China wakiwa kazini kwa sasa barani Afrika. Aidha, China imekuwa ikijihusisha ipasavyo katika upatanishi wa masuala muhimu barani Afrika, na kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa katika matukio mbalimbali kuzingatia zaidi na kutoa msaada mkubwa kwa juhudi za Afrika katika kutatua masuala ya amani na usalama.

Kuanzia kupendekeza Mpango wa Usalama Duniani hadi kuunda Andiko Dhana yake, China imezingatia kikamilifu shauku ya usalama wa nchi za Afrika. Miongoni mwa vipengele 20 vya kipaumbele vya ushirikiano vilivyoorodheshwa katika Andiko Dhana, utapata vipaumbele kama vile kuunga mkono juhudi za usalama za nchi za Afrika, Umoja wa Afrika na mashirika ya kikanda, kusaidia nchi za Afrika katika kuimarisha uwezo wao wa kulinda amani kwa uhuru, na kusaidia kushughulikia masuala muhimu ya Afrika kwa njia ya kiafrika.

Andiko hilo pia linasisitiza haja ya kutekeleza kwa vitendo Mtazamo wa Amani na Maendeleo katika Pembe ya Afrika uliopendekezwa na China, na kutekeleza jukumu muhimu la Baraza la Amani na Usalama la China na Afrika, kwa lengo la kuzingatia zaidi sababu ya amani na usalama barani Afrika na kusaidia Afrika kufikia lengo la "Kunyamazisha Bunduki" mapema.

Tanzania ni nchi muhimu katika Afrika Mashariki na ina jukumu muhimu katika masuala ya amani na usalama Afrika. Kufurahia urafiki wa jadi, China na Tanzania zimekuwa zikisaidiana kithabiti katika kulinda mamlaka, usalama na maslahi ya maendeleo, na kudumisha mawasiliano na ushirikiano katika kutatua masuala muhimu ya kikanda, hivyo kwa pamoja kutoa mchango muhimu kwa amani ya dunia.

China inatarajia kutumia fursa ya utekelezaji wa Mpango wa Usalama Duniani kuimarisha ushirikiano na Tanzania katika nyanja ya amani na usalama, kushirikiana na Tanzania kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiusalama za mila na zisizo za mila, na kulinda kwa pamoja maslahi ya jumla ya idadi kubwa ya watu wa Afrika, nchi na mataifa mengine yanayoendelea.

**•Mwandishi ni Balozi wa China nchini Tanzania.**



## Tanzania yatia saini mkataba wa SADC

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, amesema Tanzania imekuwa nchi ya kwanza kutia saini mkataba wa kuridhia kuanzishwa kwa kituo cha huduma za kibinadamu na operesheni za dharura cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ajili ya utekelezaji wa usimamizi wa shughuli za maafa nchini.

Kituo hicho kiko Nacala, Jimbo la Nampula, Msumbiji na kilizinduliwa Juni, 2021 na Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, Filipe Nyusi.

Akizungumza juzi kwenye hafla ya utiaji saini jijini hapa, Waziri Simbachawene alisema lengo la kuanzishwa kwa kituo hicho ni kusimamia masuala ya huduma za misaada ya kibinadamu kwa nchi wanachama zitakazokumbwa na maafa.

Waziri alisema malengo mengine ni kuimarisha na kuendeleza ushirikiano na uhusiano mwema baina ya nchi wanachama,kuimarisha uwezo wa kikanda wa kukabiliana na maafa pamoja na kudumisha undugu.

Lengo lingine ni kuimarisha usalama wa watu na mali katika ukanda ikiwemo kujenga mazingira rafiki ya shughuli za maendeleo na hatimaye kukuza uchumi wa Jumuiya.

"Tunaishukuru sana serikali yetu kwa kuridhia kuanzishwa kwa kituo hiki,hii itasaidia katika utekelezaji wa shughuli hizo," alisema Simbachawene.

Alisema mkataba huo umepitishwa na kamati zote zinazohusika, ikiwamo kamati ya mawaziri wanaohusika na usimamizi wa maafa Aprili, 2022 Lilongwe, Malawi, kamati ya mawaziri wanaohusika na usimamizi wa sheria na wanasheria wakuu Julai, 2022 Lilongwe.

Alisema serikali inaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maafa nchini kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa ya mwaka 2004, Sheria ya Usimamizi wa Maafa namba 6 ya mwaka 2022.

Mwanasheria Mwandamizi wa Sekretarieti ya SADC, Dk. Phineas Matto, aliishukuru serikali kutokana na kuridhia kusaini mkataba huo ambao ni muhimu kwa nchi yetu katika kukabiliana na majanga mbalimbali ya maafa.

Alisema uwepo wa kituo hicho utasaidia sana kutoa msaada wa huduma za kibinadamu katika nchi husika pale majanga yanapotokea.

# Mfumo wa GePG waongoza kukusanya mapato

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUMO rasmi wa ukusanyaji fedha za umma (GePG), umesaidia kuongeza mapato ya serikali na kudhibiti mianya iliyokuwapo awali wakati wa matumizi ya vitabu, imeelezwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Mhandisi Benedict Ndomba, alibainisha hayo juzi jijini hapo, alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mamlaka hiyo kwa waandishi wa habari.

Ndomba alisema mfumo huo umekuwa msaada mkubwa kwa serikali katika kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa mapato na kuondoa mianya yote ya watu kukwepa kufanya malipo ya serikali.

"Mfumo huu umeisadia serikali kuongeza mapato lakini pia kuona kiasi cha fedha ambacho kinakusanywa kila siku kupitia mfumo huu hata muda huu ukitaka kuangalia ni kiasi gani kimeingia unaona moja kwa moja tofauti na ilivyokuwa awali wakati tunatumia vitabu vya stakabadhi," alisema.

Pia alisema mfumo huo unaisadia serikali kutambua ni taasisi gani ambazo zimekuwa zikiongoza kwa ukusanyaji mapato nchini. "Lakini pia mfumo huu unaisaidia serikali kupata takwimu za kila halmashauri, taasisi na kutambua kuwa ni eneo gani ambalo limekuwa linachangia kwa kiasi kikubwa kwenye pato la taifa," alisema.

Kadhalika, alisema mamlaka hiyo imeendelea kusanifu, kujenga na kusimamia uendeshaji wa mifumo inayotumiwa katika taasisi za umma kwa pamoja.

"Baadhi ya mifumo hiyo, kwa mujibu wa Ndomba, ni pamoja na mfumo wa baruapepe serikalini (GMS) ambao unaziwezesha taasisi za umma kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa usalama, haraka na kwa gharama nafuu. Jumla ya taasisi 616 zinatumia mfumo huu," alisema.

Mfumo mwingine, alisema ni wa ofisi mtandao (e-Office) ambao jumla ya taasisi 200 zinautumia hadi sasa.

Vilevile, alisema mfumo wa Ofisi Mtandao mbali na kurahisisha utendaji kazi katika taasisi za umma pia umesaidia kupunguza matumizi ya karatasi na kutunza mazingira na kuokoa fedha za serikali.

"Mfumo wa Utoaji Huduma za Serikali kwa Simu za Mkononi (MGov) mfumo wa mGOV umeunganishwa na watoa huduma wote wa simu za mikononi nchini Tanzania, hadi sasa, taasisi zaidi ya 275 zimeunganishwa na kuutumia mfumo wa mGOV kutoa huduma," alisema.

Hata hivyo, alisema baadhi ya huduma hizo ni jumbe fupi yaani SMS za ununuzi wa umeme (LUKU) na SMS za huduma za malipo ya serikali.



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma juzi, kuhusu vijana 812 waliochaguliwa kujiunga na programu ya 'Building Better Tomorrow Youth Initiative in Agribusiness (BBT-YIA)', iliyopangwa kuanza Machi 17 mwaka huu katika vituo 15 vilivyoandaliwa nchini. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Mtandao barabara bora waongezeka

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MENEJA wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Lusako Kilembe, amesema barabara zenye hali nzuri zimeongezeka kutoka kilometa 699.625 hadi 1,925.084 ndani ya miaka miwili.

Akizungumza jana jijini hapa, Mhandisi Kilembe alisema ongezeko hilo ni sawa na asilimia 175.16.

Barabara zenye hali ya wastani, alisema zimeongezeka kutoka kilometa 2098.875 hadi kufikia kilometa 2755.844 sawa na ongezeko la asilimia 31.3.

"Barabara zenye hali mbaya zimepungua kutoka kilometa 4197.75 hadi kufikia kilometa 2860.92 sawa na punguzo la asilimia 31.8," alisema.

Mhandisi Kilembe alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23 bajeti ya Sh. bilioni 52.16 imetengwa ili kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara.

Alisema uboreshaji huo wa miundombinu ya barabara umesaidia usafirishaji wa mazao, watu na bidhaa kutoka sehemu moja hadi nyingine, umeimarika na kusaidia kuongeza uchumi wa wananchi wa mkoa wa Dodoma.

Pia alisema ujenzi wa madaraja umepunguza tatizo la usafiri maeneo ya vijijini ambayo yalikuwa hayafikiki kirahisi.

Aidha alisema Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) katika Mkoa wa Dodoma katika mwaka wa fedha 2020/21 ulikuwa na chanzo kimoja tu cha fedha kutoka serikali kuu kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Hata hivyo alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 na 2022/23 Wakala umekuwa na vyanzo vya fedha vitatu ambavyo ni bodi ya mfuko wa barabara, fedha za tozo ya mafuta na fedha kutoka serikali kuu.

Alibanisha kuwa fedha hizo zimeuwezesha wakala kuongeza matengenezo ya barabara, ukarabati na uboreshaji wa barabara ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita.

Alisema ongezeko hilo la mapato ya wakala umesaidia ongezeko la ujenzi wa baadhi ya barabara za lami na changarawe kwa halmashauri za Dodoma Jiji, Kondoa, Kongwa, Bahi, Mpwapwa Chemba na Chamwino.





# Rais aagiza maboresho huduma sekta ya utalii

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewataka wadau kwenye sekta ya utalii kuboresha huduma ili ziendane na mazingira ya wakati uliopo na kukidhi haja na mahitaji ya wageni wanaoitembelea Tanzania.

Dk. Mwinyi aliagiza hayo alipofungua tamasha la utalii na biashara 'The Z- Summit' kwenye Ukumbi wa Golden Tulip, Uwanja wa Ndege, Wilaya ya Mjini Unguja.

Alisema sekta ya utalii Zanzibar yenye vivutio vingi, ni muhimu na inachangia asilimia 30 ya mapato ya Zanzibar.

Alisema serikali yake inafanya jitihada mbalimbali kuimarisha sekta hiyo ili kuongeza watalii kufikia 850,000 ifikapo mwaka 2025, tayari ikiwa imeimarisha miundombinu ikiwamo kutanua barabara za kisasa na kuboresha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Alisema kwa sasa uwanja huo unatoa huduma za kimataifa zenye kukidhi haja ya mahitaji ya wageni chini ya uongozi wa taasisi ya kimaifaifa ya DNATA inayotoa huduma za kimataifa za viwanja vya ndege.

Alisema ujenzi wa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Pemba unaotarajiwa kuifungua Pemba kiutalii, ni miongoni mwa juhudi za serikali katika kukuza sekta ya utalii nchini.

Alisema Zanzibar ni kituo cha wageni wengi kutoka mataifa mbalimbali kutokana na kilivyopambwa na magofu yaliyohifadhi historia pamoja na mji mkongwe ulio kwenye hifadhi ya UNESCO unaowavutia wageni wengi kupitia fukwe na ukijani wa visiwa vyake vilinavyopambwa na michezo ya baharini.

Akizungumzia Sera ya Uchumi wa Bluu na Utalii, Dk. Mwinyi alisema serikali imechukua jitihada kubwa kuitekeleza sera hiyo kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kutilia mkazo suala la endelevu kupitia sera yake ya 'Utalii kwa Wote'.

Aliahidi kuwa serikali itaendelea kuwawekeza mazingira mazuri wadau wote wa utalii na kuwaomba mkutano huo uwe chachu ya kutoa fursa nyingi kwa watalii na wadau wake.

Alisema ni imani yake kwamba mkusanyiko huo ulioshirikisha wadau mbalimbali wa sekta, utatoa mafanikio mazuri katika kuikuza sekta nchini.

"Sote kwa pamoja tuungane kubadilishana uzoefu, kufanya kazi pamoja, tutachangia kuikuza sekta ya utalii Tanzania," alihimiza.

Akizungumzia utunzaji mazingira endelevu, Rais Dk. Mwinyi alisema utalii ni chachu ya uchafuzi wa mazingira, hivyo aliitaka jamii, wadau wa utalii pamoja na wawekezaji kwenye sekta hiyo, kutunza mazingira na viumbe vya bahari, kuepuka uharibifu wa ikolojia, uharibifu wa ardhi, uchafuzi wa hewa na maji kwa kuweka mazingira ya utalii endelevu.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, alisema kwa kuzingatia hali ya utalii ilivyo duniani, Tanzania ina kazi kubwa ya kuitangaza nchi kimataifa kupitia sekta ya utalii.

Alisema lengo lao sasa ni kuongeza watalii wengi kutoka mataifa makubwa duniani wakiwamo wa kutoka barani Ulaya, Asia, Mashariki ya Mbali na Amerika.

Pia alisema wana lengo la kuliteka soko la utalii kutoka China ambao wanaongoza dunia kutoa watalii wengi hadi kufikia milioni moja na nusu kwa kila mwaka nchini.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Muhammed Said alisema wakati umefika kwa Zanzibar kubadili mtazamo kupitia misimu ya utalii kuondokana na dhana msimu mdogo na mkubwa badala yake wawe tayari kuutangaza utalii misimu yote iwanufaishe.

Mwenyekiti wa ZATI ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii, Rahim Baloo alisema mkutano huo umelenga kuitambulisha dunia na kuitangaza Zanzibar kiutalii na kiutamaduni pamoja na kuwakaribisha wawekezaji zaidi.



Katibu Mkuu wa Jumuiya ya 'Zanzibar Outreach Programme (ZOP)', inayotoa huduma za afya vijijini, Dk. Nofal Kassim Mohammed (katikati), akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mombasa, jijini Zanzibar jana, kuhusu uzinduzi wa gari maalum la kutoa huduma za afya katika maeneo ya mijini na vijijini. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Basi la kisasa kutoa huduma tembezi za afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Zanzibar Outreach Programme (ZOP) inayotoa huduma za afya maeneo ya vijijini, Dk. Nofal Kassim Mohammed amesema wanatarajia kuzindua gari la kisasa ambalo litatoa huduma za afya maeneo ya mjini na vijijini Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mombasa, Zanzibar jana, kiongozi huyo alisema kuwa basi hilo lililotengenezwa Dubai, limegharimu dola za Kimarekani 50,000 (Sh. milioni 117) na linatarajiwa kuwasili nchini mwezi huu.

Alisema kuwa basi hilo litazinduliwa na Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui Machi 4 mwaka huu kwenye bustani ya Zanzibar Park Welezo, likiwa na mfumo wa kliniki inayotembea.

Katibu huyo alisema ujio wa basi hilo maalum lenye vyumba vya kuchunguza afya na kutibu, ni hatua muhimu inayolenga kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi wa vijijini kwa kuwafuata waliko ili kupata matibabu.

Alisema gari hilo ni la aina yake ambalo lina vyumba na vifaa muhimu vya kufanyia uchunguzi wa maradhi ikiwamo shinikizo la damu, kisukari, meno na koo.

Mjumbe wa Bodi ya ZOP, Salma Said alisema jumuiya hiyo pia imeandaa shindano la kuchora nembo ya utambulisho itakayochapishwa katika gari hilo, ikilenga kuwaibua Wazanzibari wenye uwezo ili wafahamike na kunufaika na vipaji vyao. Alisema wachoraji wanaotaka kuwania tuzo hiyo wameanza kujisajili kwa njia ya mtandao, huku akiwataka kuwasilisha kazi zao katika ofisi za jumuiya hiyo Februari 26 mwaka huu pamoja na kupata maelekezo mengine.

Alisema uzinduzi wa basi hilo utaambatana na utoaji huduma za kiafya, akiwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kupima afya zao ili kubaini kama wanazo changamoto za maradhi badala ya kusubiri kuugua.

## Serikali yapata dawa ya kumaliza migogoro ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Zanzibar, Rahma Kassim Ali amesema ardhi yote ya Zanzibar itapimwa ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuepusha migogoro na kutambuliwa na kutengwa kwa ardhi kwa shughuli za kilimo na makazi.

Amesema kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa kumesababishwa na wananchi kununuwa ardhi bila kufuata sheria na kufanya mambo kienyeji.

Waziri huyo alisema hayo juzi alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi za wizara hiyo kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2022 mbele ya Kamati ya Mawasiliano na Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi huko Maisara, Unguja.

Alisema asilimia 80 ya migogoro ya ardhi inasababishwa na wananchi kufanya ununuzi wa ardhi bila kufuata utaratibu kwa mujibu wa sheria.

Alisema ununuzi wa ardhi usiozingatia sheria pia unasababisha ujenzi holela unaokwenda kinyume cha mipango miji na makazi.

Alisema wizara tayari imefanya mikutano mbalimbali na taasisi zinazoshughulikia masuala ya utoaji wa vibali vya ardhi kwa ajili ya kuliangalia suala hilo na kudhibiti matukio hayo.

"Tayari tumefanya mikutano na taasisi mbalimbali zinazotoa vibali vya ujenzi ikiwamo Mamlaka ya Vitega Uchumi na Uwekezaji (ZIPA) pamoja na Wizara ya Kilimo kuona vibali vinatolewa na taasisi moja tu," alisema.

Akifafanua wizara tayari imetilia saini makubaliano na kampuni ya Propertie kwa ajili ya kushirikiana kupima ardhi kwa ajili ya shughuli za ujenzi na makazi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi, Sabiha Filfil Thani aliitaka Wizara kuhakikisha Mahakama ya Ardhi inatekeleza majukumu yake ikiwamo kuongeza kasi ya kuzipatia ufumbuzi kesi za ardhi zilizofikishwa na wananchi.

Alisema wakati umefika sasa kuona Wizara ya Ardhi inayapima maeneo yote ya ardhi, yakiwamo ya viwanda ambayo yamevamiwa na wananchi na kujengwa nyumba na mengine kuwauzia watu kinyume cha sheria na taratibu.

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ilibainisha kuwa kuanzia Julai hadi Desemba mwaka jana, jumla ya kesi za migogoro ya ardhi 108 zilikuwa zimepokelewa kwenye Mahakama ya Ardhi kwa ajili ya kusikilizwa.



**HARMONIZE**
UKURASA 13

Nipashe BT
JUMAMOSI FEBRUARI 25, 2023



# IMEFIKA MWISHO
## Subiri 'Season' 2...

FILAMU inayoendelea kuchezwa ya uhusiano wa kimapenzi kati ya wanamuziki wawili nyota nchini, Diamond Platnumz na Zuchu, imefika sehemu inayovutia hisia kali.

Watu waliokuwa wakifuatilia uhusiano wa wasanii hao, wamejikuta wakihitimisha ghafla baada ya kutangaziwa penzi la wawili hao limekatika ghafla.

Bosi huyo wa WCB alithibitisha kuvunjika kwa mahusiano yake na Zuchu, siku moja baada ya wawili hao kuonyesha ishara za uhusiano kati yao umeisha.

Katika kurasa za Instagram, za kila mmoja aliweka bayana kwamba penzi lao limekwisha na kilichobaki ni kama kaka na dada.

Zuchu hata hivyo hakutoa maelezo zaidi kuhusu taarifa hiyo mpya na kuwaacha mashabiki wake wakiumiza vichwa kufikiria nini kimemkuta msanii huyo.

Hata hivyo, baadhi ya mashabiki wao walionekana kutoamini maneno hayo na kueleza hiyo ni moja ya filamu yao wanayoicheza kila kukicha ili kuwapata mashabiki wengi wanaowafuatilia.

Katika maoni yao, mashabiki hao walisema kuwa wamewekwa katika mchezo huo siku nyingi bila ya kujua, na hivyo hata filamu hiyo inapotangazwa kumalizika wanachofahamu itaibuliwa tena siku si nyingi.

BASI SAWA

## Dogo Janja atazirai siku hiyo



MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Dogo Janja anatarajiwa kukumbuka mengi baada ya kuonana uso kwa uso na aliyekuwa mkewe Irene Uwoya.

Wawili hao ambao kila mmoja yupo kivyake kwa sasa wanatarajiwa kuwa pamoja katika shoo itakayowakutanisha wanamuziki na waigizaji wa Bongo muvi mkoani Kilimanjaro.


Nini kitatokea baada ya wanandoa hao walioachana kukutana kwa mara ya kwanza? Majibu yatapatikana baada ya shoo hiyo kuisha.

## Duval ndo uache kuwachimba

MCHEKESHAJI wa nchin i Marekani Lil Duval, amewakasirisha mashabiki wa muziki wa Hip hop, baada ya kutabiri kupotea na badala yake muziki wa Afrika kushika nafasi yake.

Watu waliojitokeza kutoa maoni yao katika ujumbe wa msanii huyo, walionekana kukerwa na kauli hiyo na kumtaka kubadili kauli yake.

Baada ya shinikizo kali, Duval aliandika kwenye Twitter, "Sikuwa nikisema hip hop imekwisha nilisema 'hip hop kama tunavyoijua nikimaanisha kama ilibadilika kuwa kitu kikubwa zaidi," alifafanua na kutuliza hasira.





## Diamond amfanyia makubwa mama yake

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, amefanya kufuru baada ya kumnunulia mama yake Sanura Kassim, saa ya gharama kama zawadi. Mama Dangote alionyesha saa hiyo aina ya Hublot Geneve, na kueleza kwamba mwanawe alimnunulia.

Saa hiyo inayokadiriwa kuwa na gharama ya zaidi ya shilingi milioni tisa, imekuwa miongoni mwa vitu vya thamani anavyomnunulia mama yake kila wakati.

# Walimwengu: Ubaya ndani ya dunia

**Na Adam Fungamwango**

UPO msemo wa kiswahili unaosema dunia siyo mbaya, ila walimwengu ndiyo wabaya. Walikuwa na maana kuwa dunia yenyewe hii sehemu tunayoishi haina ubaya wowote. Ila wanaoishi ndani ya dunia ambao ni wanadamu ndiyo wabaya.

Ukienda mbali zaidi unakutana na watu wanaozama ndani sana wakidai, binadamu ndiyo kiumbe hatari zaidi duniani kuliko hata mnyama yoyote yule.

Kwa haraka haraha unaweza kuwakatilia hilo. Yaani binadamu ni hatari kuliko chatu, simba, kiboko, au nyati? Lakini ipo siku isiyo na jina unaweza kukubaliana na usemi huo. Ni kwa sababu binadamu amepewa akili na Mwenyezi Mungu kuweza kuwahimili na kuwadhibiti wanyama hao. Lakini binadamu huyo huyo huitumia akili yake aliyopewa na Mungu vibaya, kuwaumiza binadamu wenzake.



Hebu soma kisa hiki cha kusikitisha kilichopo kwenye filamu iitwayo, 'Walimwengu'. Imechezwa na Haji Adam, Amne Fundi, Idd Tukutu, Azza Kipeneli na imetungwa na Zainabu Mgomba.

Haji na mkewe Azza wanadaiwa kodi ya nyumba na mama mwenye nyumbani wao anayeitwa Mama Mjengo. Anawapa siku tatu wawe wamekabidhi pesa, la sivyo wafungashe na kuondoka.

Siku hizo tatu kwao ni mtihani mkubwa, kila wanapozunguka kukopa au kuazima pesa wanashindwa kufanikiwa. Pamoja na kubembeleza Mama Mjengo, anakataa.

Mke wa Haji anakwenda kwa shoga yake wa mwisho kujaribu bahati ya kukopa pesa. Baada ya kumwambia tatizo, Amne akawapa ufumbuzi kuwa yeye hana pesa, lakini kama ni nyumba ya kuishi anayo. Wahamishe vitu vyao tu, kwani nyumba ile yote anaishi peke yake.

Inakuwa ni habari nzuri kwa Haji na mkewe. Wanahamia kwa dada Amne. Wanaishi kwa amani na utulivu. Anawaambia kuwa nyumba ile amerithi kutoka kwa wazazi wake, na yeye hajajaliwa kuolewa na hana mtoto.

Haji anapata wazo baya la kutaka kumuua Amne ili nyumba yeye na mkewe wawe warithi wa nyumba hiyo. Awali mkewe Azza anakataa, lakini kila muda unavyozidi kwenda na yeye tamaa inamuingia. Wakasahau wema wa Amne. Wakamuendea kwa mganga na kumsababishia ugonjwa wa kupooza. Wakamshinikiza awarithishe mali. Amne akakataa akidai kama akifa ameshaandika usia nyumba hiyo itolewe wakfu. Mwisho wa siku baada ya kuumwa sana, Amne anafariki.

Haji na mkewe wakadhani wamemaliza kazi. Wakaanza kuishi kwenye nyumba kama mali yao. Mzimu wa Amne unawatokea na kuwaambia japo amefariki lakini nyumba hiyo si mali yao kwa sababu alishaandika itolewe wakfu, akawaangaliza wote wawili mtu na mkewe, kabla ya mzimu huo nao kurudi ulikotoka.





## Harmonize hataki kumsikia Kajala

MKALI wa muziki wa kizazi kipya, Harmonize, ameonyesha hataki tena kusikia suala la mapenzi yake na Kajala Masanja.

Katika kile kinachoonekana kila kitu kimekwisha, amefuta tattoo zote zenye majina ya Kajala na mwanawe Paula ambazo aliziandika kwenye mguu wake.

Wakati akitambulisha singo yake mpya inayoitwa 'Single Again', ameonekana kwenye video akiwa hana tattoo hizo ambazo huko nyuma zilikuwa zikionekana zikitanda mguuni mwake.

## INAUMA, UTANIUA KAMA ZUWENA

**Na Adam Fungamwango**

NI mwezi wa mapenzi. Ni mwezi wa makopakopa. Februari mara nyingi huwa ni mwezi wenye pilikapilika nyingi za mapenzi. Kilele chake huwa ni tarehe 14, lakini wengine yanaendelea kwa wapenzi kutumiana zawadi na kubebishana mwezi mzima.

Kwenye masuala ya burudani, umekuwa ni mwezi wa moto. Wasanii mbalimbali, mastaa na chipukizi wamekuwa wakipishana studio kutoa ngoma.

Mastaa wote wakubwa unaowajua, mwezi huu walijifungia studio na kuipua ngoma ambazo zimebamba mtaani na kuwa gumzo.

**ZUWENA-DIAMOND PLATNUMZ**

Picha tu linaanza, Februari 3 staa na kioo wa muziki wa kizazi kipya nchini, Diamond Platnumz anatoa ngoma yake aliyoiita 'Zuwena'. Hii ngoma ina mambo mengi sana kwa sababu ilianza kusikika kabla hata haijatoka. Ni kwa sababu huyu msichana aliyecheza kama queen kwenye video hii, alianza kuwa maarufu na hata baada ya ngoma hiyo kutoka ameendelea kuwa maarufu mno. Imeshatazamwa na watu milioni 8.9 mpaka sasa kwenye mtandao wake wa instagram.

Maudhui ya wimbo huu ni jamaa aliyefiwa na kaka yake miaka kadhaa iliyopita, akaenda kuzuru kaburi lake na kama utamaduni wa Kiafrika ulivyo. Unaweza kufika kaburini na kuongea, ukimuelezea marehemu maisha unayoishi duniani. Waafrika wengi wanaamini kuwa marehemu waliofariki zamani wanakuwa mizimu ambao wanaweza kusikia na kusaidia unachoomba.


Ndiyo maana mtu hata maisha yake yakiwa mabaya au kuna kitu anahitaji, anaweza kwenda kwenye makaburi ya wazazi wake kama wamefariki na kuomba.

Diamond kwenye ngoma hii anamwambia kaka yake wote ni wazima, ila mali zote na pesa alipewa Zuwena, lakini baada ya kupata amebadilika kabisa. Zuwena wa jana si wa leo. Kwa sasa amekuwa sistaduu, anayeyajua ya usiku na ya mchana.

**INAUMA-ASLAY**

Siku hiyo hiyo ya Februari 3, msanii Aslay naye akafyatua ngoma yake aliyoiita 'Inauma'. Jamaa ambaye ameachana na mpenzi wake, lakini hata wiki haijaisha ameshapata bwana. Sasa hili limeonekana kumkera sana Aslay, anaanza kulalamika. Anaona kama ndiyo hivyo basi huyo mpenzi wake mpya alikuwa naye tangu zamani, maana haiwezekani uachane na mwenzi wako, binti ameshapata mwingine na hata haonyeshi majonzi yoyote. Anatanua tu na kipenzi chake kipya.

**UTANIUA-ZUCHU**



Wiki moja baadaye, Februari 10, mmoja kati ya wasanii bora kabisa wa kike, aliyetoka kwenye familia ya wanamuziki wa taarab, Zuchu, akatoa ngoma yake iitwayo 'Utaniua'. Ni ngoma ya mapenzi, ambayo ameitoa kwenye mfumo wa audio, bado hajatoa video yake.

"Baby mimi hata taabani, wewe utaniua." Ni moja kati ya maneno yaliyomo kwenye ngoma hiyo.

**SINGLE AGAIN-HARMONIZE**

Tembo wa muziki wa kizazi kipya Tanzania, Harmonize, yeye alitoa ngoma yake siku nne tu baada ya Zuchu kutoa ya kwake. Ilikuwa ni Februari 14. Ngoma yake ina historia ya kweli ambayo imemtokea yeye mwenyewe. Ameiimba kwa lugha ya kingereza, ikiwa bado kwenye mfumo wa 'audio', akiita 'Single Again', akiwa na maana 'bachela tena.'

Siku chache tu kabla ya kutoa ngoma hiyo aliweka bango kubwa pale Mnazi mmoja, likiwa na maneno ambayo ni jina la wimbo huo. Imetazamwa na watu kiasi cha milioni 1.6 kwenye mtandao wake wa instagram mpaka sasa.

Ametunga ngoma hii baada ya kuachana na mpenzi wake msanii wa filamu, Kajala Masanja hivi karibuni.

**MAHABA-ALI KIBA**

Huyu ni mtaalam mwingine wa muziki wa kizazi kipya nchini, Ali Kiba. Siku tatu tu baada ya Harmonize kutambulisha ngoma yake hiyo, yeye akaja na pini yake ambayo ni kama vile maudhui yanataka kufanana 'Mahaba'.

Kiba anasema siku hizi hakuna mapenzi, kuna mapenzi ya mkataba ambayo baada ya siku kadhaa yanakwisha, Mapenzi yanachosha, yanaumiza na ni bora tu ampende aliyemzaa. Hii ndiyo Februari ya makopakopa inayomalizikia.




# Nadia amshukuru AKA

MPENZI wa rapa wa Afrika Kusini, AKA, Nadia Nakai, ameandika ujumbe mzito kama heshima ya marehemu mpenzi wake.

Nakai, ambaye alikuwa mpenzi wa rapa huyo hadi alipouawa kwa kupigwa risasi wiki iliyopita, alilalamika kwa uchungu, kuwa hakutegemea kama hayo yangemkuta.

"Moyo wangu umevunjika, hii sio jinsi maisha yetu ya baadaye yalivyokuwa. Siamini kuwa jana niliaga kwaheri yangu ya mwisho. Sitakuona tena kwa muda wote. Ulinipenda kwa sauti kubwa, fahari. Asante mpenzi wangu," ameandika.



## Muuaji wa Nipsey apatikana na hatia

ERICK Holder, Jr. ambaye ni mshtakiwa wa mauaji ya rapa Nipsey Hassle, amekutwa na hatia ya kuua kwa kiwango cha kwanza.

Ermias Asghedom maarufu Nipsey Hussle alipigwa risasi na kufa papo hapo nje ya duka lake Jijini Los Angeles Mwaka 2019.

Kwa mujibu wa Wakili wa Utetezi, Holder alimshambulia mshindi huyo wa tuzo mbili za Grammy kwa risasi mara 10 na baadaye kumpiga teke la kichwa kwa madai kuwa alihisi Hussle anashirikiana na polisi.

## R Kelly aanza kutumikia miaka 50

MWANAMUZIKI nyota wa Marekani, R Kelly, ameanza kutumikia adhabu nyingine ya miaka 20 jela iliyotolewa juzi na mahakama ya mjini Chicago.

R Kelly amepewa adhabu hiyo baada ya kupatikana na hatia ya makosa ya Ponografia na kushawishi watoto kushiriki shughuli za uhalifu wa kingono.

Tayari msanii huyo anatumikia kifungo kingine cha miaka 30 jela kwa unyanyasaji wa kijinsia.

Jaji Harry D. Leinenweber amesema katika miaka 20 aliyohukumiwa, 19 itaenda sambamba na hukumu ya miaka 30 kisha mwaka mmoja uliosalia atautumikia baada ya kumaliza kifungo cha miaka 30.





## Phyna kumbe alinusurika kifo

MSHINDI wa Big Brother Naija, Ijeoma Otabor, anayefahamika zaidi kwa jina la Phyna, amefichua tukio la kulishwa sumu.

Phyna amefichua tukio hilo ambalo limewashtua mashabiki wengi, wakati wakitoa maoni yao na kuuliza kuhusu afya yake.

Phyna alihoji kwanini kuna mtu anamchukia kiasi cha kutaka kumuua.

"Niliokolewa baada ya kutaka kula sumu. Sijawahi kumuudhi mtu yeyote, nina moyo safi na roho safi kwa nini chuki nyingi dhidi yangu? Mungu aliniokoa," ameandika.

## Yul wape ushauri, wakipinga shauri yao

Mwigizaji maarufu kutoka Nigeria, Yul Edochie, amewaonya watu kufikiria hatma ya nchi yao na kuacha vitendo vya vurugu wakati wa uchaguzi.

Amesema kila Mnigeria anatakiwa kuwa makini na watu wanaogombea, ikiwa kuchunguza kauli zao kwani inapotokea vurugu watakaoumia ni watu wa hali ya chini

"Kila mgombea anahitaji kukushawishi katika sanduku la kura, wanatumia kila aina ya maneno kuwavutia na pale wanapotaka mtoto wenu kuwaunga kwenye magenge sema hapana," ameandika Edochie.





## Wananchi kunufaika na uhifadhi wa misitu

**Na Steven William,** MUHEZA

MRADI wa miaka mitatu wa kuimarisha usimamizi wa ushoroba wa bioanuai ya Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asili ya Amani na Msitu wa Hifadhi wa Nilo, unaotekelezwa na Kikundi cha Uhifadhi wa Misitu Tanzania (TFCG), utawanufaisha wananchi wa vijiji 18 wanaovizunguka.

Ofisa Mradi huo kutoka TFCG, Ewald Emil, alisema mradi huo una lengo la kuunganisha misitu hiyo na kutoa elimu kwa wananchi juu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira yake ili yasiathiriwe na mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea duniani kote.

Emil alizungumza hayo jana, wakati wa kuutambulisha mradi huo kwa wataalam wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga.

"Tutaanza na kuvijengea uwezo vijiji 12 kati ya 18 vinavyopitiwa na mradi huu. Kimsingi, mradi huu wa miaka mitatu unaotambulishwa ulianza kutekelezwa Novemba 14 mwaka 2022 na utatekelezwa hadi Novemba mwaka 2025.

"Kwenye mradi huu, kuna program ya kuwajengea uwezo wanafunzi katika utunzaji wa mazingira. Programu hiyo inaitwa Eco Schools," alisema.

Alisema kuwa mradi huo unatekelezwa na TFCG, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na wadau wengine mbalimbali wa misitu ikiwamo Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Aidha, mwezeshaji wa mradi huo, Joneth Mbogo, alisema kuwa mradi huo unajihusisha na kufanya kazi na wadau mbalimbali kwa kutoa elimu ikiwamo wanaotengeneza majiko sanifu na kutoa hamasa katika Michezo ili watu wajue utunzaji wa mazingira.

Baada ya utambulisho huo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina, alisema wakazi wa Wilaya hiyo, wameupokea mradi huo kwa mikono miwili.

"Niagize sasa, wataalam wote na watendaji mtoe ushirikiano mzuri ili wenzetu hawa wa TFCG wafanikishe malengo yao katika uhifadhi wa misitu katika Wilaya ya Muheza," alisisitiza Mhina.

# Walimu wabanwa madai ubakaji, ulawiti

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SAKATA la madai ya ulawiti na matukio mengine ya ukatili wa kingono kuzihusisha baadhi ya shule mkoani Kilimanjaro, limesababisha Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kutangaza marufuku ya walimu wa shule za umma, kuvaa suruali za 'jeans' shuleni na walimu wa kike kuvaa nguo fupi na za kubana mwili, kuanzia Machi Mosi, mwaka huu.

Aidha, Jeshi la Polisi limeagiza kila shule za sekondari na msingi wilayani hapa kuanzisha vitengo vya intelijensia ya wanafunzi na madawati ya jinsia shuleni ili kukabiliana na vitendo vya ulawiti na ukatili.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa wazazi na walezi wa wanafunzi wanaosoma katika Shule ya Sekondari ya Kimochi, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Moris Makoi, alisema mwalimu atakayebainika kuvunja makubaliano hayo atakuwa ameingia katika mgogoro wa kimaadili na serikali, hivyo kuhatarisha ajira yake.

"Halafu hizi lifti ndizo zinazotuumizia watoto. Ukipita huko barabarani hawaendi nyumbani wanasubiri lifti ya mtu wasiyemjua wala kuwa na ahadi naye, hivyo atapata mimba tu. Malori ya mchanga yanapakia wanafunzi mpaka kibini inajaa, uharibifu tayari na sijui wanawapeleka wapi?

"Mzazi sema na mwanao, mwambie ukweli ulimwengu ulipofika na yeye anatakiwa achukue hatua gani. Wako walimu wanajihusisha na mapenzi na watoto shuleni, wako watoto nao wamekengeuka wanatoka kimapenzi na walimu.

"Mtumishi ambaye hataki kuvaa mavazi ya staha kwa mujibu wa maelekezo ya serikali na sheria zetu za utumishi wa umma, huyo hatufai. Haiwezekani wewe unamfundisha mtu na huku unamharibu. Mwalimu hawezi kuinama, lakini anawaambia watoto wainame. Kuna haki hapo?," alihoji.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kimochi, Chrispine Njinji, aliwasihi wazazi wa wanafunzi wa shule hiyo, kupunguza harakati za kutafuta maisha, badala yake wawafuatilie watoto wao kuhusu dalili za ulawiti na ukatili mwingine dhidi ya watoto.

"Kuanzia sasa, tunafuta matumizi ya mavazi ya vibamba, kuvaa viatu bila soksi, wanaume kushona suruali za kubana hips ili flaizi isifunge. Hatutaki kuyaona katika shule hii, kwa sababu hizo ni dalili za wanafunzi kuingia katika uchafu unaotajwa wa ushoga na ulawiti.

"Yuko mwanafunzi amepata ujauzito hapa shuleni kwetu na kukatisha masomo yake, baada ya kukosa sabuni ya kufulia, mwingine mama yake mzazi alimfukuza nyumbani akamwambia hana sukari, kwa hiyo akatafute sukari kilogramu moja amlete bila ya kumpa pesa. Mwanafunzi huyo akarubuniwa na kijana mmoja, akapewa shilingi 3,000 ya sukari na akapewa ujauzito siku hiyo hiyo," alisema.

Kutokana na kashfa hiyo, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Criss Makere, aliyemwakilisha Mkuu wa Ushirikishwaji Jamii wa Polisi Wilaya ya Moshi, ASP Juma Kabelwa, aliagiza wakuu wa shule, kuanzisha vitengo vya intelijensia ya wanafunzi, kwa kuchagua wanafunzi wanaoweza kuwafuatilia kwa siri wenzao wanachokifanya na kuwaripoti ili kuukabili ulawiti shuleni.




Meneja Mauzo wa Vodacom Tanzania Wilaya za Moshi na Rombo, Kanankira Nanyaro (kulia), akikabidhi kompyuta kwa Mwalimu wa Shule ya Sekondari Sakayo Mosha, Ivan Temu wakati wa hafla fupi shuleni hapo, mkoani Kilimnajro juzi. Vodacom imetoa msaada wa kompyuta kwa shule 16 za mkoa huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawekezaji walia kukatika kwa umeme

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MAUMIVU ya kukatika kwa umeme mkoani Tanga, yamewaibua wawekezaji wa viwanda vinavyotumia malighafi ya klinka, kuzalisha bidhaa za ujenzi na kubainisha kuwa uzalishaji unashuka kutokana na kuzalisha kwa hasara.

Malalamiko ya wawekezaji hao yaliwasilishwa jana kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba na Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Neelkant kilichoko Amboni, Rashid Liemba.

Akizungumza na Mkuu wa Mkoa, aliyetembelea kiwanda hicho, Liemba, alisema tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara, limekuwa kikwazo kikubwa katika uzalishaji malighafi kwenye viwanda vikubwa na vidogo.

"Hili tatizo linasababisha uzalishaji kukosa tija. Katika katika hii ya umeme bila taarifa inaathiri sana shughuli zetu za uzalishaji viwandani. Tunakuomba mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ufuatilie hili ili walau tuzalishe kwa tija na si hasara," a lisema Liemba

Kuhusu kiwanda cha kuzalisha kadi za vitambulisho na vocha, Liemba alisema hivi sasa wako kwenye mchakato wa kuanza uzalishaji.

"Kiwanda hiki kwa sasa kipo katika mchakato wa kuanza kuzalisha. Tunazalisha kadi za benki mbalimbali na kadi za NIDA (vitambulisho vya taifa), hivyo tunaomba serikali itupe msaada wa kututafutia oda katika masoko. Tukishapata tupo tayari kuanza uzalishaji," alisema Liemba.

Aidha, Meneja wa Kiwanda cha Kuchakata Mkonge cha Amboni Spinning Mill Ltd, Robert Semwaiko, alisema serikali ina wajibu wa kutatua kero za wawekezaji, kabla hawajakata tamaa na kushindwa kufanya uzalishaji.

Semwaiko alisema hivi sasa kuna ukakasi mkubwa katika suala la kamba za katani wanazotengeneza na zile za plastiki kutoka nje, ambazo zimeonekana kufifisha biashara ya kamba zao.

Akijibu malalamiko hayo, Mgumba alisema serikali imepokea kero hizo na itazishughulikia haraka iwezekanavyo ili viwanda hivyo viendelee kustawi na kuzalisha kwa tija.

"Nimekuja kuwasikiliza, kukagua shughuli zenu zinaendeleaje na kusikiliza kero zenu ili tuzitatue kwa pamoja.

"Nia ya serikali ni kuona ustawi wa viwanda unarudi katika nafasi yake. Mkistawi ninyi na wengine wengi watakuja kuwekeza, lakini mkiwa mnalialia, hakuna mwekezaji atakayekuja kuwekeza katika mkoa huu," alisema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Hadithi za zamani bila sungura hainogi

## • Rafiki yake fisi ni lazima awe bwege
## • Zimwi lilisababisha woga kwa watoto

**Na Adam Fungamwango**

KUTOKANA na maendeleo ya teknolojia watoto wengi hivi sasa wanapenda sana kuangalia filamu za katuni. Katuni hizo ambazo mara nyingi ni za wanyama wa aina mbalimbali ambapo watoto hufurahi wanavyowaona, wanavyoongea, kutembea, kula na vituko mbalimbali wanavyofanya.

Zamani haikuwa hivyo. Filamu za katuni za enzi hizo ilikuwa ni watoto kusimuliwa hadithi na wakubwa waliowazidi umri.

Ila kwa kumbukumbu na uzoefu wangu, wapiga hadithi mara nyingi huwa si baba. Mababa wa zamani mara nyingi hawakuwa na urafiki wa karibu kivile na watoto wao, na hata wa jirani zao.

Mara chache huwa ni kila mama kusimulia watoto wao. Ila watu waliokuwa wasimuliaji wakubwa ni wenye umri mkubwa, kama vile babu au bibi.

Nadhani hawa kwa sababu mara nyingi hawakuwa na kazi kubwa za kufanya, wengi wameshastaafu. Walipenda kukaa na wajukuu zao na kuanza kuwasimulia au kupigia hadithi za mapokeo.

Watoto waliokuwa wakiishi mijini walikuwa wakipata wasaa huo wanapokwenda vijijini wakati wa likizo ambako wanakutana na babu na bibi zao.

Wengine ambao hawapati nafasi za kwenda huko, husimuliwa na watu waliowazidi umri ambao wanaishi maeneo ya jirani.

Wakati mwingine babu na bibi nao huwa wanatembelea watoto zao mijini na kukutana na wajukuu zao, hapo lazima hadithi zipigwe.

Watoto waliozaliwa vijijini ndiyo kabisa, wao husimuliwa hadithi na babu na bibi zao ilikuwa ni kama ada, wakati mwingine ilikuwa ni kila siku baada ya chakula cha jioni.

Hadithi za mapokeo ni nini? Ni simulizi ambazo zimerithiwa toka enzi na enzi, kizazi kwa kizazi. Kizazi kimoja kimekuwa kikisimulia kizazi kingine, nacho kinaendelea kuwasimulia wengine, hivyo kupokewa na kuendelea kusimuliwa miaka na miaka kila inavyozidi kusonga mbele.

Ilipokuja teknolojia ya vitabu, hadithi hizo zilianza kukusanywa na kuwekwa kwenye vitambu mbalimbali. Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) miaka ya 1980 hadi 1990 ilikuwa na kipindi kilichoitwa 'Mama na Mwana' ambapo pamoja na mambo mengine ya watoto ilikuwa ikisimulia hadithi mbalimbali za kusisimua za mapokeo, ikiwa na watangazaji wake mahiri wakati ule, Debora Mwenda na baadaye Sara Dunda.





Waafrika wana hadithi nyingi za mapokeo ambazo lengo lake ilikuwa ni kuburudisha, kufundisha, kudumisha tamaduni, ikiwemo kuwaepusha watu na matatizo yanayoweza kuwakabili kwa kuwatia hofu. Ndiyo maana kuna hadithi zingine huwa ni za kutisha sana kiasi kwamba baadhi baadaye walikuwa wakiweweseka usiku na kupiga kelele.

Hadithi nyingi zilikuwa ni za kufikirika ambazo hazikuwa na ukweli wowote, lakini zilitengenezwa au kutungwa kwa sababu nilizoeleza hapo juu na ziliisaidia sana jamii hasa kwa kipindi kile.

Ndiyo maana kulikuwa na kitu kinaitwa zimwi. Ni jitu la kufikirika, ambalo kwa mujibu wa hadithi za mapokeo linaelezwa kuwa lina umbile kubwa kuliko binadamu wa kawaida. Lina sura mbaya isiyotazamika, muonekano unaotisha, wakati mwingine kuna mkia kama mnyama. Hata hivyo hadi naandika makala hii sijawahi kuliona jitu hilo linaloitwa zimwi au hata kusikia mtu yoyote ameshawahi kukutana nalo.

Hii ilitengezwa kwa ajili ya kuwatia hofu watoto ili wawe kwenye msitari. Lakini hilo lilisababisha, watoto wengi kuogopa hata kutoka nje usiku kwenda msalani, akihofu huenda anaweza kukutana na hilo jitu. Mfano kuna hadithi moja ya mapokeo ya msichana aliyekataa kuolewa na wanaume wote wa eneo hilo. Sababu hazijulikani. Lakini akatokea mwanaume mmoja kutoka mbali ambaye hajulikani mwenye muonekano mzuri aliyefika kumchumbia. Msichana alikubali, lakini alikuwa na mdogo wake wa kiume ambaye aliomba kwenda naye huko atapokwenda dada yake. Familia ilikataa, lakini mume alikubali kumchukua. Haikuwa kama walivyodhani. Mwanaume huyo hakuwa binadamu wa kawaida. Alikuwa zimwi, alijigeuza binadamu wa kawaida kwa ajili ya kwenda kumuoa msichana yule. Lengo halikuwa ndoa ila kumla nyama. Baada ya miezi minne sasa msichana alinawiri na kunenepa. Mume alikuwa akitoka asubuhi kwenda shambani. Siku moja shemeji yake alimfuata. Akamuona shemeji yake amebadilika na kuwa zimwi akiimba 'wamenenepa sasa, shime ni chakula changu'. Kijana akakimbia upesi nyumbani na kumweleza dada yake ambaye alipinga kuambatana naye alikoolewa, wakatoroka haraka sana kabla zimwi halijaja. Kumbe zimwi lililazimisha shemeji aende kwa sababu tayari alikuwa na nyongeza ya nyama. Hadithi hii iliwafundisha mabinti kutokuwa na tabia ya kuchagua na kuwakataa wachumba, pia kutokubali wachumba ambao hawawatambui sawa sawa, walikotokea, au tabia zao.

Inafundisha pia kutokuwa na roho mbaya kwa ndugu kwani msichana ameolewa na ndugu yake ambaye alikuwa amekataa asiongozane naye.

Kwenye hadithi za mapokeo za wanyama kama hakuwepo sungura, hiyo hadithi basi itakuwa na upungufu na watoto hawatoifurahia.

Kwenye hadithi za wanyama watoto walimpenda sungura kwa sababu alihadithiwa kama mnyama mtundu, mwerevu, mwenye akili nyingi, mjanja na mwenye kila aina ya hila. Kwenye hadithi zote alikuwa akiwapelekesha wanyama wote wakubwa kama simba, chui, kifaru, ngiri, tembo.

Na hadithi hizo za wanyama hao wanaoongea na kuishi kama binadamu, haikamiliki bila ya kumuweka mnyama fisi. Huyu ndiye anayefanywa bwege na kuonewa na sungura mara kwa mara. Ametengenezwa kama mnyama mwenye tamaa, mchoyo, mjinga, na mlafi.

Ipo hadithi ambayo sungura na fisi waliambizana wawachinje mama zao kwa sababu wameshakuwa wazee. Sungura akaenda kumficha mbali mama yake, fisi akamchinja kweli. Kilichotokea ni kwamba fisi alikufa kwa njaa kwa sababu hakuwa na wa kumpikia, wakati mwenzake anakwenda kula kwa kificho kwa mama yake, akiimba na kufunguliwa mlango.

Kuna hadithi moja ambayo sungura na fisi walikwenda ugenini, lakini njiani wakaamua kujipa majina, sungura akajipa jina la 'chawageni' na mwenzake akazugwa kupewa jina la 'chawote'.

Kilichotokea kila siku kikipikwa chakula na kupelekewa, sungura anawauliza wenyeji, hiki ni cha nani? Wanajibu chawageni. Sungura anakula peke yake.

Kali kuliko yote fisi alikula nyama yote waliyokwenda kuwinda wakati sungura alipokuwa amelala. Akaongopa imegeuka mkaa wakati wa kuchomwa kwa sasa hata yeye alipitiwa na usingizi.

Sungura alifahamu hila ya fisi. Siku moja walikwenda kuiba ndizi, sungura alimpiga mwenzake na marungu bila kufahamu, akijifanya yeye ni mlinzi wa migomba hiyo.

Siku ya ngoma kwa mfalme Simba, fisi alianza kuimba, 'nyama nimekula nimeongopea mkaa', sungura naye akajibu,'nimekupiga migombani nimeongopea askari'. Ugomvi wake hapo ukawa si wa kawaida.

**Tuma meseji 0716 350534**



HABARI KIMATAIFA

## Polisi Indonosia yazima vurugu

**JAKARTA,** INDONESIA

VIKOSI vya usalama vya Indonesia viliimarisha ulinzi katika mji wa Wamena katika eneo la mashariki mwa Papua, baada ya watu tisa kuuawa wakati wa ghasia zilizochochewa na uvumi kwamba mtoto alitekwa nyara.

Msemaji wa polisi wa jimbo la Papua, Ignatius Benny Adyolisi, alisema wanausalama wapatao 200 wamepelekwa kudhibiti hali ya usalama baada ya watu 14 kujeruhiwa katika ghasia za juzi.

Ghasia katika eneo hilo zilizuka baada ya wenyeji kuvurumisha mawe kwenye kituo cha polisi cha Wamena ambacho kinamshikilia mtu anayetuhumiwa kumteka nyara mtoto wa miaka sita.

Hata hivyo polisi imesema hali ya utulivu imeimarishwa. **DW**

## Mgombea akutwa na mfuko uliojaa pesa za kuwahonga wapiga kura

**ABUJA**, NIGERIA

MGOMBEA wa ubunge nchini Nigeria amekamatwa kwa madai kukutwa na pesa taslimu dola 498, siku moja kabla ya uchaguzi mkuu unaofanyika leo.

Polisi walikuta kitita cha pesa hizo za kimarekani ndani ya gari la Chinyere Igwe, ambaye ni mwanachama wa chama cha upinzani cha PDP na mgombea wa Baraza la Wawakilishi.

Aidha, alinaswa akiwa na orodha ya watu waliotakiwa kupewa pesa hizo kabla ya kwenda vituo vya kupigia kura.

Katika chaguzi zilizopita, wanasiasa wameshutumiwa kwa kununua kura.

Nigeria imeunda upya sarafu yake ya Naira, ili kudhibiti na kufanya iwe vigumu kwa wanasiasa kukusanya kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kuwahonga wapiga kura.

Hata hivyo, noti mpya hazitoshi, jambo linalosababisha hasira kwa wananchi. Watu wamekuwa wakipanga foleni kwa saa nyingi nje ya benki ili kupata pesa, lakini wengi wanaondoka bila kufanikiwa.

Asilimia 40 ya Wanigeria hawana akaunti za benki na hivyo wanategemea pesa taslimu kununua chakula, na kwa matumizi mengine ya kila siku.

Katika mtandao wa Twitter, polisi wa Jimbo la Rivers waliwataka wagombea wote na vyama vya kisiasa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi na sheria zingine za nchi.

Uchaguzi huo unatabiriwa kuwa wenye ushindani mkubwa zaidi tangu kumalizika kwa utawala wa kijeshi mwaka 1999, huku wagombea watatu wakionekana kuchuana vikali. **BBC**

# Chui awajeruhi watu 13

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

CHUI mmoja amewashambulia watu 13 wakiwemo watoto katika mji wa Alaba Kulito, nchini Ethiopia.

Tukio hilo limetokea umbali wa kilomita 200 kusini mwa mji mkuu Addis Ababa, kabla ya mnyama huyo kupigwa risasi na polisi katika msako uliodumu kwa saa kadhaa.

Taarifa zilieleza kwamba mara ya kwanza kuwa mnyama huyo alivunja nyumba majira ya asubuhi na kuanza kuwashambulia watu.

Hata hivyo, vikosi vya polisi vilitumwa kwenda eneo hilo kwa ajili ya kudhibiti hali hiyo.

"Alikuwa anaruka juu ya paa la nyumba. Jambo ambalo lilizua taharuki katika jamii. Chui huyo aliyekuwa na hofu akaanza kuwashambulia watu," Naibu Kamanda wa Polisi Taju Negash aliambia BBC.

Miongoni mwa waathirika walikuwa watoto wawili, wanawake na wengine vijana.

Haijajulikani chui huyo alitoka wapi, lakini polisi walisema waliojeruhiwa wanatibiwa hospitalini.

Tukio kama hilo lilitokea Septemba mwaka jana, chui aliua mume na mke waliokuwa wakirejea nyumbani na kuwajeruhi wanamgambo wawili huko eneo la Jimma, magharibi mwa Ethiopia.

Wataalamu wanaonya kuwa mashambulizi ya wanyama yanaongezeka kutokana na baadhi ya watu kujenga nyumba katika maeneo karibu na makazi yao ya asili.

**BBC**



Wanajeshi wa Ukraine wakirusha kombora kupitia mtambo wa M777 Howitzer, wakiwa mstari wa mbele kuongoza mashambulizi dhidi ya vikosi vya Russia katika Mkoa wa Kharkiv. **PICHA: REUTERS**

# Russia yaendelea kubanwa vita Ukraine

**NEWYORK,** MAREKANI

UMOJA wa Mataifa umetoa wito wa kuwepo kwa amani na haki ya kudumu na kuitaka Russia kuondoa wanajeshi wake na kuacha mapigano nchini Ukraine.

Wito huo umetolewa siku moja baada ya mwanadiplomasia mkuu wa China, kuitembelea Russia na kuahidi ushirikiano zaidi.

China haijapiga kura kwa mara ya nne kupinga hatua ya Russia kuivamia Ukraine Februari 24 mwaka jana.

Azimio hilo lilipitishwa Alhamisi kwa kura 141 za ndio na 32 hazikuhudhuria.

Nchi sita ziliungana na Russia kupiga kura ya hapana, Belarus, Korea Kaskazini, Eritrea, Mali, Nicaragua na Syria.

Naibu Balozi wa Russia katika Umoja wa Mataifa Dmitry Polyanskiy, alipuuza hatua ya kura hiyo na kuiita isiyokuwa na maana.

"Je, italeta amani? Hapana! Je, itawatia moyo wachochezi wa vita? Ndiyo! Hivyo hii ni kurefusha janga la Ukraine." alisema.

Russia ililitaja azimio hilo kuwa lisilo na usawa na chuki dhidi ya nchi yao na kuzitaka nchi kupiga kura ya hapana ikiwa haziwezi kufanyiwa marekebisho.

Mshirika wa Russia, Belarus alishindwa katika jaribio hilo la kubadilisha maandishi na marekebisho ikiwa ni pamoja na kuzuia kuongezeka zaidi kwa mzozo kwa kuwapa wahusika silaha.

Mataifa ya Magharibi yameipatia Ukraine silaha za mabilioni ya dola tangu Russia ilipovamia.

Marekani na NATO katika wiki iliyopita waliishutumu China kwa kufikiria kusambaza silaha na kuionya dhidi ya hatua hiyo.

Wakati huo huo, Idara ya Sheria ya Marekani imejumuisha katika orodha ya vikwazo kwa zaidi ya vyombo 80 vya kisheria, pamoja na makampuni ya Kichina ambayo yanashukiwa kuunga mkono sekta ya ulinzi ya Russia.

Utawala wa Biden hivi majuzi umeibua wasiwasi kwamba China inaweza kuiuzia Russia silaha moja kwa moja.

Gazeti la Ujerumani Der Spiegel, liliandika kwamba Russia inajadiliana na China kuhusu ununuzi wa ndege zisizo na rubani za kamikaze.

Hata hivyo, China inakanusha mpango huo.

Aidha, Uingereza imeongeza idadi ya watu wanaokabiliwa na vikwazo katika orodha yake ikiwa ni pamoja na - wawakilishi wa msafara wa Putin na mameneja wakuu 34 wa Russia wanaohusishwa na kampuni zinazomilikiwa na serikali.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIDNEY SAUL NDEKI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 328 AFM – SUZUKI SJ. Chassis namba JSA0SJ40V00564484. Engine namba F10A678327. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/74572/2023.**

## TANGAZO! TANGAZO! TANGAZO!



**LAH: KUCHUKULIWA KWA NDUGU JOSHUA SIMON SUKI ALIYECHUKULIWA NA WATU WASIOJULIKANA**

FAMILIA YA **SIMON YOHANA SUKI** NA **FAMILIA YA MCHUNGAJI RAPHAEL MAKWALE** ILOYOKO **MASWA** MKOA WA **SIMIYU** INAWATANGAZIA KUWA MNAMO TAREHE **23/12/2022** MAJIRA YA SAA **11:00** JIONI NDUGU **JOSHUA SIMON SUKI** MKAZI WA **MASWA MJINI** ALIFIKIWA NA WATU WASIOJULIKANA DUKANI KWAKE NA KUMCHUKUA NA KUONDOKA NAYE NA KUELEKEA KUSIKOJULIKANA.

NDUGU HUYO ALIKUWA AMEVAA TISHETI YA MIKONO MIREFU RANGI YA KIJIVU YENYE MISTARI MWEUSI NA JINSI YA RANGI YA BLUU NA CHINI ALIKUWA AMEVAA RABA ZA RANGI YA KIJANI PIA ALIKUWA NA AMEVAA KOTI LA KIJANI.

HIVYO FAMILIA INAOMBA MSAADA KWA MTU YEYOTE ATAKAYEMWONA ATOE TAARIFA SAHIHI ZA KUMPATA **KITUO CHA POLISI** KILICHOKO KARIBU NAWE AU AWASILIANE NA FAMILIA KWA NAMBA ZIFUATAZO: –

**+255 784 004 111 / +255 766 693 168 / +255 766 054 477**

ZAWADI YA KIASI CHA **TSH. 1,000,000/– (MILIONI MOJA)** ZITATOLEWA NA FAMILIA KWA ATAKAYEFANIKISHA KUMPATA NDUGU YAO.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya CHAMWINO MJINI**
**Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO**
**Mkoa DODOMA**
**Shauri a madai/Ndoa Na 58/2022**
**Jina la Mdai: ABDALLAH JOHN**
**Jina la Mdaiwa: ISRAEL MWANGWEMBE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: ISRAEL MWANWEMBE**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake YA **TSH. 2,000,000/-**(milioni mbili tu)
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katikaMahakama hii **Tarehe 01 Mwezi 03 Mwaka 2023 saa 7.00** mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo..
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe **13 Mwezi 02 Mwaka 2023**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJILI

**MALILA DICKSON ELIA** Anatangaza kupotea kwa cheti cha usajili cha Taasisi ya **ROUNDING HANDS TO SAVE THE COMMUNITY** Kilichosajiliwa mnamo Tarehe **23.08.2019** chenye Namba ya Usajili **OONGO/R/0532.** Kwa yeyote aliyekiona awasiliane na namba : **SIMU NAMBA: 0756 545910**
Au atoe Taarifa polisi: TAARIFA NAMBA: **IRI/IRI/RB/74800/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZUAKUU GODSON KALAGHE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T 979 AGY – TOYOTA HILUX. Chassis namba LN1060091605. Engine namba 3L3173183. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/74992/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORA HUSSEIN MNDOLWA** Anatangaza kupotolewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T. 634 DML aina ya TOYOTA KLUGER. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi: **KAH/RB/142/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LAURENSIA JOSEPH MABOMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 945 AVN – TRAILER. Chassis namba MICL02508. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /827/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHAIBU ISSA ALLY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 787 AFG – MAZDA**. Chassis namba UFYDF3244987. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /789/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BONIFAS J. ALLON** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 587 AYQ – TOYOTA. Chassis namba SXN100046530. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /782/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GRIVAS DICKSON MWANGOKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 388 AUC – MITSUBISHI.** Chassis namba **FE638E532512.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /780/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NITIKE N. MWAMBENE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 677 CEM – HAQJUE. Chassis namba LC6PCJK27J0079318. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB /304/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi na 42|2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HASHIMU HASSANI**
**KATIKA SHAHURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIOLETWA NA SALUMU HASHIMU HASSANI**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama zamwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa
Hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehem anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetotewa leo tarehe 24 Mwezi 02 mwaka 2023

HAKIMU

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI NA.81/2022**
**LUCIA DANIEL MWANG'OMBE::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**1.ENITAR SAINETI MWANGILE:::::::::::::MDAIWA**
**2.SAMSON DANIEL MWANG'OMBE::::::MDAIWA**

**YAH:KUITWA SHAURINI**

**KWA:SAMSON DANIEL MWANG'OMBE**
Fahamu kwamba **LUCIA DANIEL MWANG'OMBE** amefungua shauri dhidi yako katika Baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 27/02/2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo,baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 16/01/2023.

**T.Munzerere**
**MWENYEKITI**
**16/01/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

**BRANDINA AGEN ELISA** Anatangaza kupotelewa kwa Hati ya kiwanja kilichopo kiegea chenye utambulisho wa namba PLOT NO. 327 BLOCK J "KIEGEA" Yenye majina ya ELIZABETH YUDA LEKULE.Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu au piga cm no **0768554345. MOR/MOR/RB/74879/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI,**
**IDARA YA UHAMIAJI.**


**OFISI YA UHAMJIAJI MKOA**
**SLP 404,**
**IRINGA**
**21.02.2023**



**HII NI TAARIFA KUWA**
**BW. PINKALKUMAR HASMUKHBHAI PATEL**
Mwenye picha yake imeonyeshwa hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Yeye ni raia ya India nan chi atokayo ni India na kazi yake/Muajiriwa katika Kampuni ya TOP SHOP LIMTED –IRINGA. Ameishi nchini tangu 2010 na kwa sasa anaishi IRINGA-MJINI.
Mtu yeyote mwenye sababu yakupinga Muombaji asipewe uraia, atume taarifa yake ya Maandishi iliyos sainiwa kwa:

**KAMISHINA GENERALI WA UHAMIAJI,**
**SLP 1181,**
**DODOMA**
**PROPERTY NUMBER: WPC/20432/21**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**YUSTA SELEMANI MIMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S0924-0055** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **IKUNGI SEKONDARI** mwaka **2016**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DAR/KIL/RB/44291/2023**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# MTAKE MSITAKE-20

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa kipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kiburi cha kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yanayopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja ya wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Tatizo wewe binti unajifanya mjanja. Mimi nilikutaka siku nyingi sana. Ukanikataa tena kwa maneno mabovu. Leo umeona umuhimu wangu eee? Sasa mimi hili swali kwangu ni dogo mno kuliko kuua panzi, nzi au mbu. Ni kiasi cha kukaa naye kumpa mzigo tu, yaani pesa kidogo, tunaiua hii skendo humu humu kijijini, haitoki nje. Lakini kwa sharti moja tu." Safari hii aliongea kwa sauti kidogo ya msisitizo.

"Mimi niko tayari kwa sharti lolote utakalonipa, lakini hili liishie humu."

"Nataka unikubalie, niwe mpenzi wako."

"Mimi sina neno na hilo. Niko radhi, ila tu itabidi univumilie kidogo."

"Kuna nini tena?" Akang'aka.

"Nilikuwa na matatizo ya tumbo, nikaenda hospitali, nikapimwa na kupewa dawa za kutumia ambazo naendelea kuzitumia. Sasa waliniambia nisifanye kitu chochote kwa miezi mitatu. Ikiisha tu basi tutaanza rasmi uhusiano,"

"Imeisha hiyo. Mimi kesho tu nitakwenda kwa mzee Chale. Hana tatizo yule anapenda pesa tu, nikimpa milioni zake mbili tu, atanyamaza. Halafu shoo nasimamia mimi mwenyewe. Nitamwambia habari hii haitakiwi kuvuka kijijini hapa."


"Nitashukuru sana."

"Kama kweli umenikubali, hebu naomba nikubusu."

***************************

Sauti hizo za kurekodiwa ziliwashangaza wanakijiji waliokusanyika hapo, huku kila mmoja akishangaa juu ya mpango mkakati uliofanywa na Adel pamoja na Mary kumhadaa Usonzo na akahadaika.

"Nadhani mmesikia hapo. Baada ya hapo ni kama Usonzo alikuwa ameshamaliza kazi ya kumhitaji Mary kuwa mpenzi wake. Alichokuwa anakifanya ni kusubiri hiyo miezi mitatu. Tulipofanikiwa hili, tukaendelea kumfanyia ulaghai. Nikamwambia Mary amdanganye anataka kuishi naye, lakini siyo hapa. Na kabla ya hilo ahakikishe anatoa pesa ya kunisafirisha kwenda Dar nikatibiwe na macho yangu yatapona. Kwake Usonzo ilionekana kama mimi ndiyo nadanganywa ili nikatelekezwe Muhimbili ili yeye na Mary watoroke. Nalo hilo akaingia mkenge. Hebu niwasilizishie tepu hii ambayo Mary alikuwa anaongea na Usonzo."




**"Yaani kwa plani yote uliyoifanya nakupa mia kwa mia, hata kesho mlete nimwambie mimi nitamgharamia kila kitu, safari pamoja na matibabu."**

*****************************

"Nimekwambia nimetumia njia hiyo ili akubali kunyamaza na kutokwenda kushtaki. Kumbuka yule kwao ni Dar es Salaam ambako kuna kila kitu, anaweza kwenda huko akashtaki wakaja maaskari kutoka Kituo cha Kati Dar. Nimemwambia asishtaki na nimemwambia pia nitamgharamia gharama za matibabu Dar es Salaam ili wakafanye uchunguzi huenda yanaweza kuona tena. Baada ya kumwambia hivyo amekubali. Nikatoka hapo, nikaenda hadi kwa ndugu zake, maana mtu anaweza kukubali, lakini ndugu zake wakapinga. Nao nimewatuliza kwa kuwaambia kuwa ndugu yao anaweza kupona kwa kumpeleka Dar kwa matibabu zaidi, lakini ukweli ni kwamba hawezi kupona au kuona maisha yake yote daktari amethibitisha."

"Sasa anaondoka lini huku kwenda kwenye matibabu feki atuondolee jinamizi sisi huku?"

"Usonzo, jambo hili ni kubwa, usilione ni rahisi rahisi, limekaa kimitego sana. Yule kwa sasa nakaa naye nyumbani ili asishawishiwe na mtu kubadili mawazo akaenda kushtaki. Yeye anaamini kuwa atakwenda Dar kutibiwa atapona, na baada ya hapo ndiyo tutaanza kuwa wapenzi..."

"Ahaa, yaani umemdanganya akishatibiwa ndiyo mtaanza rasmi uhusiano?"

"Sasa je. Mpango huo hata mchumba wangu Enock anaujua na kuuelewa, ingawa sijamwambia hilo jambo la kumkubalia kuwa mpenzi."

"Du, msichana una akili wewe, yote haya kakufundisha nani? Yaani wewe Mafia."

"Ngoja, sikiliza sasa, ndiyo nakuja huko."

"Enhee, lete habari mpenzi."

"Kwa maana hiyo pia ninaomba kiasi cha pesa kidogo ili nikawapelekee ndugu zake hapa kijijini kama rushwa wasiongeeongee sana. Halafu nataka nimlete kwako, ili umwambie kuwa wewe utagharamia matibabu yake yote mjini. Unajua tayari ameshanza kuniuliza wewe pesa zote utatoa wapi? Nimemwambia nina wadau wangu watanisaidia."

"Yaani kwa plani yote uliyoifanya nakupa mia kwa mia, hata kesho mlete nimwambie mimi nitamgharamia kila kitu, safari pamoja na matibabu."

"Sawa ila subiri muda wa kumuondoa hapa utakuwa ule ambao nilikwambia tutaanza rasmi uhusiano. Miezi mitatu ijayo."

"Halafu tunampeleka Dar, Muhimbili tunamtelekeza."

"Sawa kabisa."

"Ila nina swali hapo kidogo Mary?"

"Lipi tena Usonzo na wewe?"

"Kama akitoka huko na kusema waliomtelekeza si anaweza kuja na polisi huku?"

"Sasa hapo tutakuwa wapenzi kamili kazi kwako baba."

"Basi nitakuhamisha hapa, nitakupeleka Arusha ukale kuku. Wakija hapa hola."

*******************************

Adel akazima kitufe cha tepu hiyo na kuendelea kuuangalia umati ambao ulionekana kuchangamka, huku wengine wakionekana kupongezana na kufurahia mbinu ambazo Adel na Mary walizifanya kuwaaminisha watu kuwa mmoja kamwagia mwenzake tindikali kwa lengo la kumpumbaza Usonzo lakini pia kumrahisishia kufanya uchunguzi au upelelezi.

"Ndugu wanakijiji, mpango ulikwenda kama tulivyopanga, sasa tukapanga kwenda ofisini kwa Usonzo. Yeye alijua kuwa mimi nimepelekwa pale ili kudanganywa kuwa nitapelekwa Dar kwa matibabu lakini nitaona, lakini lengo ni kwenda kutelekezwa kama ambavyo walipanga na Mary ili watoroke. Lakini alikuwa hajui kuwa Mary alinipeleka ofisini hapo kwa kazi moja tu ya kumpeleleza, huku mwenyewe akijua mimi sioni.

Humo ndani baada ya kuzungumza naye na alituacha kwa muda wa saa zaidi ya nzima. Na hilo lilikuwa kosa kubwa kwake. Kwanza Mary alinisaidia kurekodi mazungumzo kama kawaida, lakini mimi nilipiga picha nyaraka zote muhimu alizokuwa amehifadhi ofisini mwake, lakini nilivyofoa baadhi kwa ajili ya ushahidi ambao ninaono na tutaupeleka mahakamani kuonyesha kuwa aliingia mikataba feki ya kuhodhi ardhi ya wanakijiji kwa njia ya udanganyifu. Siku ambayo tulikwenda na Mary ofisini mwake mazungumzo yalikuwa kama ifuatavyo. Akabonyeza tena kitufe kuwasikizishia wanakijiji mazungumzo ya siku hiyo Mary alipokwenda na Adel kwenye ofisi za Usonzo kufanya upelelezi bila yeye kujua.

*********************************

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# CHAMA: SIMBA TUNAENDA KUPINDUA MEZA UGANDA

**Na Hadija Mngwai**

KIUNGO wa kimataifa wa Simba, Clatous Chama, amesema kikosi chao kimejiandaa vizuri kuhakikisha wanapata ushindi katika mechi ya leo dhidi ya Vipers FC ya Uganda ili kuwarejeshea heshima na furaha wanachama na mashabiki wao .

Vipers FC inaikaribisha Simba katika mechi ya Kundi C ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kwenye Uwanja wa St. Mary's ulioko Entebbe, Uganda.

Simba inashika mkia katika kundi lake kutokana na kupoteza michezo miwili ya awali, alifungwa bao 1-0 na Horoya AC ya Guinea akiwa ugenini halafu akapokea kichapo cha magoli 3-0 kutoka kwa Raja Casablanca ya Morocco, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, Chama, alisema baada ya kutofanya vizuri katika michezo miwili iliyotangulia, tayari wamebaini makosa na sasa wamejipanga kuongeza umakini na kucheza kwa tahadhari.

Chama alisema mechi zilizopita hawakuwa na utulivu hasa katika eneo la ushambuliaji na kuongeza kwa sasa wamejipanga kupata ushindi na kurejesha heshima, furaha na imani kwa mashabiki wao.

"Mechi mbili za kimataifa hatukuanza vizuri, tumepoteza zote, mechi hii ya tatu tunacheza ugenini, mchezo utakuwa mgumu kwa sababu hatuna hali nzuri. Kocha ametuelezea mambo mengi sana ya kuhakikisha tunapindua meza dhidi ya Vipers ili kurudisha amani na uaminifu kwa mashabiki, wasichoke kuwa na sisi," alisema Chama.

Kiungo huyo aliwataka mashabiki wao waendelee kuwapa ushirikiano na kuahidi upepo huo mbaya wanakwenda kuumaliza katika mechi hiyo ya leo.

" Watuombee, watuamini kwa sababu tunaweza kufanya vizuri, sisi ni wapambanaji, Simba ni timu kubwa na tuna kocha mzuri, watuamini lolote linaweza kutokea, tutapambana kusaka ushindi," Chama alisema.




Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya M-BET Tanzania, Allen Mushi (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya thamani ya Sh. milioni 175.3, Abdallah Segatwa, ambaye alishinda zawadi hiyo kupitia droo ya Perfect 12. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

# M-BET yaitakia heri Simba

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kampuni ya Mchezo ya Kubashiri ya M-Bet Tanzania imewazawadia washindi wawili kila mmoja Sh. milioni 175.3 baada ya kubashiri kwa usahihi matokeo ya ligi mbalimbali kupitia mchezo wa Perfect 12, imewatakia heri Simba itakayoshuka ugenini leo kuikabili Vipers katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Washindi waliopata zawadi hiyo katika hafla iliyofanyika jijini, Dar es Salaam jana ni Mesharam Bakunda na Abdallah Segatwa. Mkurugenzi wa Masoko wa M-BET Tanzania, Allen Mushi, alisema wanajisikia fahari kubadili maisha ya mashabiki wa soka ambao wote ni wafuasi wa Arsenal.

"Mbali ya kubadili maisha ya washindi wetu, pia tunajisikia fahari kuchangia asilimia 20 ya kodi ya ushindi ambayo inaigia moja kwa moja serikalini. Sisi ni walipa kodi wazuri wa serikali na tunachangia maendeleo, pia tunaitakia Simba mafanikio mema katika mchezo wake dhidi ya Vipers ya Uganda utakaochezwa leo," Mushi alisema.

Bakunda ambaye pia ni shabiki wa Yanga alisema hakuamini kushinda kiasi hicho cha fedha kwa kutumia Sh. 1,000 tu.

"Mimi mkulima, nitatumia fedha hizi kwa ajili ya kuendeleza kilimo, kuboresha nyumba na kusomesha watoto wangu. Nimekuwa nikibashiri na kupata hela ndogo ndogo. Nilipopigiwa simu na kuambiwa nimeshinda zaidi ya milioni 100, sikuamini, nilidhani ni ndoto," alisema Segatwa.

## Ilamfya afungiwa mechi 3 Ligi Bara

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Mtibwa Sugar, Charles Ilamfya, amefungiwa kucheza soka kwa mechi tatu mfululizo na kutozwa faini ya Sh. 500,000 kwa kosa la kumpiga ngumi mchezaji wa Dodoma Jiji FC, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa Februari 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro.

Naye kocha wake, Melis Medo, amefungiwa kukaa kwenye benchi la timu yake kwa mechi tatu na kulipa faini ya Sh. milioni moja, kwa kumpokonya mwamuzi kadi ya njano katika mechi hiyo na kumwonyesha mwamuzi wa akiba.

Kocha huyo alifanya kitendo hicho ambacho kimetafsiriwa ni kuchafua taswira ya ligi. Alionyeshwa kadi ya njano na mwamuzi kwa kupinga maamuzi, na kumtolea lugha isiyo ya kiuanamichezo mwamuzi wa akiba.

Baada ya tukio hilo la kupora kadi na kumuonyesha mwamuzi wa akiba, Medo alitwangwa kadi nyekundu na kuondolewa kwenye eneo la ufundi.

## Straika Kitayosce ajitabiria makubwa

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Kitayosce FC, Fabrice Ngoy, ambaye ni kinara wa kupachika mabao katika Ligi ya Championship, amesema kwa kushirikiana na wachezaji wenzake anaamini mbali na timu hiyo itapanda kucheza Ligi Kuu Bara msimu ujao huku yeye akiibuka mfungaji bora.

Nyoy ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemkrasia ya Congo (DRC), anaongoza kwa ufungaji katika Ligi ya Championship akiwa amepachika mabao 13, amefunga hat-trick moja, amesema lengo lake namba moja ni kuiwezesha Kitayosce kupanda Ligi Kuu.

Alisema anahitaji kuona pia anafikia malengo yake binafsi ya kujitangaza katika soka la Tanzania na kutwaa kiatu cha dhahabu.

"Ushirikiano uliopo na wachezaji wenzangu ndiyo unaonifanya mimi kuwa mshambuliaji bora, kufunga mabao mengi kadri inavyowezekana, nipo hapa kufunga na kuisaidia timu kushinda," alisema Ngoy.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Kitayosce iko kwenye nafasi ya pili ikiwa na pointi 41 wakati maafande wa JKT Tanzania wenye pointi 46 ndio vinara.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RICE ATAJWA ARSENAL**
ARSENAL wamemweka kiungo wa kati wa West Ham na Timu ya Taifa ya England, Declan Rice, mwenye umri wa miaka 24 kama ndio chaguo lao la kwanza kwenye usajili wa majira ya joto. ***(Football.London)***

**JUDE AISHABIKIA LIVERPOOL**
JUDE Bellingham hajakatishwa tamaa na matokeo mabaya ya hivi majuzi ya Liverpool na anasalia kushabikia klabu hiyo na kocha wake, Jurgen Klopp. ***(Athletic)***

**MIN-JAE ANUKIA UNITED**
KLABU ya Manchester United inataka kuimarisha safu yao ya ulinzi kwa kumsajili beki wa kati wa Napoli na Korea Kusini, Kim Min-jae, mwenye umri wa miaka 26, ambaye ana kipengele cha kuachiwa kwa pauni milioni 42. ***(Corriere dello Sport)***

**UNITED KUMBAKISHA GERNACHO**
MANCHESTER United ina nia ya kumpa mkataba mpya wa muda mrefu fowadi wa Argentina na mchezaji anayechezea kikosi cha umri chini ya miaka 20, Alejandro Garnacho. Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 unamalizika msimu wa joto wa 2024 na klabu inataka kumzawadia nyongeza kubwa ya mshahara. ***(Mail)***

**FABINHO KUUZWA BAADAYE**
KIUNGO wa kati wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Brazil, Fabinho, mwenye umri wa miaka 29 anaweza kuuzwa baada ya miaka mitano ya kukaa hapo Anfield huku kocha, Jurgen Klopp akitafuta kukiboresha kikosi chake msimu wa joto. ***(Mirror)***

**MADDISON AKARIBIA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inaongoza katika harakati za kumsajili kiungo wa kati wa Leicester City na Timu ya Taifa ya England, James Maddison, mwenye umri wa miaka 26. ***(Football 365)***

**LUKAKU: SIRUDI CHELSEA**
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku, mwenye umri wa miaka 29, hataki kurejea Chelsea baada ya muda wake wa mkopo katika klabu ya Inter Milan kukamilika mwishoni mwa msimu. ***(9b0 min)***

**BETO KUTUA EVERTON**
EVERTON inaweza kumnunua mshambuliaji wa Udinese, Mreno Beto, mwenye umri wa miaka 25, msimu wa joto baada ya ofa "kubwa" kwa mchezaji huyo kukataliwa Januari. ***(Liverpool Echo)***

**RAPHINHA ATAJWA ARSENAL**
ARSENAL iliwasilisha ofa ya euro milioni 70 kwa Barcelona kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 26 Januari. ***(Sport)***

**VALENCIA AELEKEA BRAZIL**
MSHAMBULIAJI wa zamani wa West Ham na Everton, Enner Valencia, anakaribia kujiunga na Internacional FC ya Brazil akitokea Fenerbahce, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ecuador mwenye umri wa miaka 33 akitarajiwa kuhama kwa uhamisho wa bila malipo. ***(Fabrizio Romano)***

**PAEZ KUTUA CHELSEA**
KLABU ya Chelsea inakaribia kufikia makubaliano ya mdomo na Independiente del Valle kwa ajili ya kumsajili kiungo wa kati wa Ecuador, Kendry Paez, mwenye umri wa miaka 15. Nyota huyo atajiunga na timu yake mpya atakapofikisha umri wa miaka 18. ***(Fabrizio Romano).***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG AWAPIGIA SALUTI NYOTA UNITED

## Kocha huyo akiri kikosi chake kimepata ushindi wa kwanza mkubwa tangu...

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag aliipigia saluti timu yake "imara" ya Manchester United baada ya kupata ushindi dhidi ya Barcelona katika mashindano ya Ligi ya Europa.

Baada ya mchezo wa kwanza kutoka sare ya 2-2 kwenye Uwanja wa Camp Nou wiki iliyopita, Mashetani Wekundu walianza kuwa nyuma kwa penalti ya Robert Lewandowski kipindi cha kwanza katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi.

Lakini kikosi cha Ten Hag kiligeuza matokeo baada ya mapumziko kwa mabao ya Fred na Antony aliyetokea benchi na kuwapeleka wenyeji kutinga hatua ya 16 bora ya mashindano hayo.

Pia ilikuwa mara ya kwanza tangu kufungwa na Granada Aprili, 2021 ambapo Blaugrana hao walipoteza wakiwa wameongoza kabla ya mapumziko.

Alipoulizwa kama huo ulikuwa ushindi wake mkubwa tangu achukue nafasi hiyo, Mholanzi huyo aliiambia BT Sport: "Ndiyo, nadhani hivyo. Tumepata ushindi mzuri – Liverpool na Arsenal nyumbani. Barcelona ndio kinara wa LaLiga, pointi nane mbele ya Real Madrid, kuwafunga ni ushindi mkubwa kwetu.

"Nadhani tuna wachezaji wakubwa kwenye timu, kama Rapha (Varane) na Licha (Lisandro Martinez), hawamwogopi mtu yeyote. Hata unapopata vikwazo, wanasonga mbele, wanaendelea na wana ujasiri. Wanataka kupata matokeo.

"Hata unapopiga penalti, lazima uendelee; unaweza kubadilisha michezo kama hii. Unaposhinda mchezo mkubwa kama huu - baada ya kuwa nyuma kwa bao 1-0 na hali ngumu - nadhani hii ni nzuri na inatoa a motisha."

Baada ya bao la ushindi la Antony, United sasa wamefunga mabao 19 kupitia wachezaji wa akiba katika michuano yote msimu huu, mabao mengi zaidi kwa upande wowote kutoka kwenye ligi kubwa tano za Ulaya.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,080,3
MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ALLEGRI: DI MARIA AMEIBORESHA JUVE



**TURIN, Italia**

KOCHA Massimiliano Allegri, amesifu kiwango cha Angel Di Maria baada ya winga huyo kufunga hat-trick na kuisaidia Juventus kuitoa Nantes na kutinga hatua ya 16 bora ya Ligi ya Europa hapo juzi.

Di Maria aliwaweka Bianconeri mbele kwa bao zuri la kwanza baada ya dakika tano tu, kabla ya kisigino chake cha nyuma kuzuiwa kuingia kwa mkono wa Nicolas Pallois, na kumfanya mwamuzi kuamua mkwaju wa penalti.

Di Maria alifunga penalti iliyotokana na Pallois na mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina akamalizia hat-trick yake kwa kichwa dakika za lala salama na kupelekea Bianconeri kusonga mbele.

Di Maria amekuwa mchezaji wa kwanza wa Juve kufunga mabao matatu katika mechi moja ya Ulaya tangu Filippo Inzaghi alipofanya hivyo mwaka 2000.

"Angel ni bingwa wa dunia," Allegri aliwaambia wanahabari baada ya mechi. "Anaongeza ubora wa Juventus hii na sote tuna furaha juu yake.

"Kuwa na mtu kama yeye ni muhimu kwa timu. Sasa, anaijua timu vizuri zaidi na yuko vizuri kimwili."

Allegri alifurahishwa na matokeo ya mechi ya mkondo wa pili ya timu yake baada ya sare ya 1-1 ya kusikitisha mjini Turin na kuifanya timu yake kuwa na mtihani mgumu wa kusonga mbele kwenye Uwanja wa de la Beaujoire.

# Xavi akiri Barca imeimarika

**MANCHESTER, England**

XAVI Hernandez alisisitiza Barcelona wameimarika licha ya kuondolewa tena mapema kwenye michuano ya Ulaya, wakati huu kutoka kwa Manchester United kwenye Ligi ya Europa, Alhamisi.

Penalti ya Robert Lewandowski ya kipindi cha kwanza iliipa Barca bao la kuongoza usiku na kwa sare, lakini mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa wachezaji wawili wa Brazil, Fred na Antony yaliifanya United kutinga hatua ya 16 bora kupitia ushindi wa jumla wa 4-3.

Iliendeleza rekodi mbaya ya Barca Ulaya katika misimu ya hivi karibuni. Wameshindwa kutoka katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika kila baada ya miaka miwili iliyopita na walitupwa nje ya Ligi ya Europa na Frankfurt katika hatua ya robo fainali Aprili, mwaka jana.

"Tumekuwa bora zaidi kuliko msimu uliopita," alisema Xavi. "Tulikuja dhidi ya Bayern (Munich), Inter na United wakati huu. Hizi ni timu kubwa na zenye nguvu, lakini hatukuwa bora vya kutosha.

"Tumeimarika, lakini haikutosha. Tutajaribu tena. Tutajikosoa na kujaribu kuwa washindani zaidi na kuangalia kuimarika Ulaya."

Baada ya sare ya 2-2 kwenye Uwanja wa Camp Nou wiki iliyopita, Barca walicheza vyema kipindi cha kwanza pale Old Trafford lakini walipoteza njia baada ya mapumziko.



## HABARI MICHEZO


318,061/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/02/23 | 18:00 | Everton FC vs Aston Villa | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 02. 25/02/23 | 18:00 | Birmingham City vs Luton Town | 2.90 | 3.15 | 2.45 |
| 03. 25/02/23 | 18:00 | Bristol City vs Hull City | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 04. 25/02/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Blackburn Rovers | 2.45 | 3.25 | 2.85 |
| 05. 25/02/23 | 18:00 | Stoke City vs Millwall FC | 2.49 | 3.15 | 2.85 |
| 06. 25/02/23 | 18:00 | West Bromwich Albion vs Middlesbrough FC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 07. 25/02/23 | 18:15 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 2.85 | 3.10 | 2.55 |
| 08. 25/02/23 | 20:30 | Schalke 04 vs VfB Stuttgart | 3.00 | 3.30 | 2.31 |
| 09. 25/02/23 | 21:00 | Maritimo Madeira vs Santa Clara Azores | 2.50 | 3.10 | 2.85 |
| 10. 25/02/23 | 22:45 | US Lecce vs Sassuolo Calcio | 2.41 | 3.20 | 2.95 |
| 11. 25/02/23 | 23:00 | Valencia CF vs Real Sociedad San Sebastian | 2.85 | 3.20 | 2.48 |
| 12. 26/02/23 | 16:30 | Tottenham Hotspur vs Chelsea FC | 2.34 | 3.25 | 3.00 |
| 13. 26/02/23 | 17:00 | FC Nantes vs Stade Rennes | 3.20 | 3.20 | 2.23 |
| 14. 26/02/23 | 17:00 | Clermont Foot 63 vs Strasbourg Alsace | 2.28 | 3.20 | 3.15 |
| 15. 26/02/23 | 17:30 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.37 | 3.40 | 2.85 |
| 16. 26/02/23 | 18:30 | Rio Ave FC vs GD Chaves | 2.55 | 3.15 | 2.80 |
| 17. 26/02/23 | 18:30 | FC Lugano vs FC Basel 1893 | 2.45 | 3.25 | 2.36 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 25/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 2172 | Coventry vs Sunderland | 2.22 | 3.22 | 3.13 |
| 16:00 | 2633 | Espanyol vs Mallorca | 2.34 | 2.90 | 3.35 |
| 16:00 | 5986 | Coastal Union vs Tanzania Prisons | 2.01 | 2.92 | 3.84 |
| 17:30 | 1102 | Werder Bremen vs VfL Bochum | 1.95 | 3.62 | 3.42 |
| 17:30 | 2549 | Hoffenheim vs Borussia Dortmund | 3.87 | 3.97 | 1.76 |
| 17:30 | 2587 | Hertha BSC vs Augsburg | 2.11 | 3.46 | 3.16 |
| 17:30 | 3128 | RB Leipzig vs Eintracht Frankfurt | 1.67 | 3.92 | 4.46 |
| 17:30 | 3626 | FC Koln vs VfL Wolfsburg | 2.33 | 3.32 | 2.87 |
| 18:00 | 1090 | Leicester vs Arsenal | 4.17 | 3.79 | 1.74 |
| 18:00 | 1135 | Aberdeen vs Livingston | 1.87 | 3.49 | 3.93 |
| 18:00 | 1614 | Bristol City vs Hull City | 2.29 | 3.22 | 3.02 |
| 18:00 | 1806 | Preston vs Wigan | 2.20 | 3.17 | 3.22 |
| 18:00 | 1909 | Portsmouth vs Cheltenham | 1.76 | 3.62 | 4.27 |
| 18:00 | 2160 | Stoke City vs Millwall | 2.37 | 3.12 | 2.97 |
| 18:00 | 2496 | Burton vs Accrington | 1.80 | 3.66 | 3.96 |
| 18:00 | 3021 | Charlton vs Sheffield Wed | 3.57 | 3.42 | 1.97 |
| 18:00 | 3692 | Barnsley vs Derby | 2.73 | 3.23 | 2.47 |
| 18:00 | 3812 | Birmingham vs Luton Town | 2.88 | 3.13 | 2.42 |
| 18:00 | 3815 | Leeds vs Southampton | 1.94 | 3.42 | 3.67 |
| 18:00 | 4027 | Norwich City vs Cardiff | 1.70 | 3.66 | 4.55 |
| 18:00 | 4068 | Sheffield Utd vs Watford | 1.84 | 3.52 | 3.97 |
| 18:00 | 4133 | Kilmarnock vs Motherwell | 2.41 | 3.19 | 2.89 |
| 18:00 | 4313 | Everton vs Aston Villa | 2.41 | 3.11 | 2.91 |
| 18:00 | 4333 | West Ham vs Nottingham | 1.73 | 3.52 | 4.56 |
| 18:00 | 4939 | West Bromwich vs Middlesbrough | 2.34 | 3.30 | 2.86 |
| 18:00 | 4956 | MK Dons vs Ipswich | 5.35 | 3.87 | 1.58 |
| 18:00 | 5127 | QPR vs Blackburn | 2.13 | 3.27 | 3.27 |
| 18:00 | 5399 | Reading vs Blackpool | 2.02 | 3.42 | 3.42 |
| 18:00 | 5962 | Burnley vs Huddersfield | 1.37 | 4.56 | 7.73 |
| 18:15 | 1546 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 2.88 | 2.98 | 2.58 |
| 18:15 | 4384 | Genoa vs Spal | 1.58 | 3.69 | 5.69 |
| 18:30 | 5803 | FC Arouca vs Casa Pia Atletico | 2.25 | 3.14 | 3.19 |
| 19:00 | 1962 | Angers vs Lyon | 4.67 | 3.77 | 1.68 |
| 19:00 | 4026 | Fenerbahce vs Konyaspor | 1.52 | 4.25 | 5.52 |
| 19:00 | 5098 | Azam vs KMC | 1.27 | 3.72 | 6.73 |
| 20:00 | 5432 | Empoli vs Napoli | 6.13 | 4.55 | 1.43 |
| 20:15 | 4839 | Racing Genk vs Oostende | 1.33 | 5.38 | 7.17 |
| 20:30 | 4605 | Bournemouth vs Manchester City | 8.31 | 5.06 | 1.31 |
| 20:30 | 4897 | Real Madrid vs Atletico Madrid | 1.78 | 3.61 | 4.31 |
| 20:30 | 4941 | Schalke 04 vs Stuttgart | 2.91 | 3.26 | 2.33 |
| 21:00 | 4488 | Maritimo vs Santa Clara | 2.13 | 3.09 | 3.54 |
| 21:00 | 5192 | Metz vs Nimes | 1.68 | 3.52 | 4.95 |
| 22:00 | 5056 | AZ Alkmaar vs Cambuur | 1.24 | 5.94 | 9.70 |
| 22:30 | 5855 | FC Zurich vs BSC Young Boys | 3.06 | 3.49 | 2.17 |
| 22:45 | 2052 | Lecce vs Sassuolo | 2.43 | 3.12 | 2.87 |
| 22:45 | 5077 | Crystal Palace vs Liverpool | 4.46 | 3.77 | 1.69 |
| 23:00 | 1320 | Montpellier vs Lens | 4.26 | 3.57 | 1.78 |
| 23:00 | 5638 | Valencia vs Real Sociedad | 3.00 | 3.15 | 2.38 |
| 23:00 | 5784 | Sporting Gijon vs Tenerife | 2.40 | 2.92 | 3.12 |
| 23:30 | 1445 | FC Vizela vs Benfica | 7.56 | 4.78 | 1.36 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# POLISI TANZANIA ITABAKIA LIGI KUU BARA - ZAHERA

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kupoteza kwa bao 1-0 kwenye uwanja wa nyumbani dhidi ya Mbeya City, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Mwinyi Zahera, amesema timu yake haitashuka daraja kwa sababu ya tofauti ya pointi chache iliyopo kati yao na klabu nyingine zilizoko mkiani.

Akizungumza mara baada ya mechi hiyo juzi, Zahera, kocha wa zamani wa Yanga, alisema hawezi kukubali tayari timu yake itashuka daraja mpaka pale kila kitu kitakaposhindikana.

Kocha huyo alisema amebakiwa na mechi sita mkononi hivyo ana uwezo wa kupata pointi 18 ambazo zitatosha kumweka salama katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Kipindi cha kwanza tulikuwa na shida ya kupoteza mpira, wachezaji hawarudi haraka, wenzetu walikuwa na kasi sana, nadhani hii inasababishwa na mechi tuliyocheza juzi dhidi ya Prisons, wachezaji walijituma sana ndiyo maana kipindi cha kwanza tulipata shida, tunaweza kubaki Ligi Kuu inawezekana sana," alisema Zahera.

Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mubiru Abdallah, alisema pamoja na kupata ushindi, bado wachezaji wake walionyesha makosa mengi.

"Mchezo ulikuwa mgumu, pamoja na ushindi tulikuwa na makosa kadhaa, tulikuwa tunapoteza mpira sana na tunakosa sana mabao, nadhani wachezaji wangu walicheza kwa presha kwa sababu hatujapata ushindi katika mechi tatu zilizopita, mechi zilizobaki tunahitaji pointi 10 tu," alisema Mubiru.



Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Temeke, Dar es Salaam, Faudhia Hamisi, akionyesha umahiri wa kucheza na nyoka wakati Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), kilipoenda kuzindua klabu ya ujasiriamali shuleni hapo hivi karibuni. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# SIMBA, VIPERS VITA YA MAJIRANI

INATOKA UK. 24

wa ikawa rahisi, tutatakiwa kujua jinsi gani ya kucheza wakati tukiwa na mpira na tusipokuwa nao. Tunahitaji ushindi kwa ajili ya klabu yetu, wanachama, mashabiki na nchi kwa ujumla, na mengine ni siri yetu, ila kwenye mechi hii nitawafanyia 'sapraizi',' alisema Robertinho.

Aliongeza watacheza kwa nidhamu kwa sababu wanawaheshimu wapinzani wao na anahitaji pointi tatu na si mabao mengi katika mchezo.

"Kwa ujumla tumepata muda mzuri wa kufanya maandalizi, lakini nafurahi kurejea kwa Kanoute ambaye alikosekana kwenye mchezo uliopita dhidi ya Raja Casablanca kutokana na kutumikia adhabu ya kadi tatu za njano," aliongeza kocha huyo.

Beki Mkenya, Joash Onyango, alisema wachezaji wote wanafahamu hawajafanya vizuri katika mechi mbili zilizotangulia kitu ambacho hakijawahi kutokea tangu aanze kuichezea timu hiyo na sasa wamerekebisha makosa yao.

Onyango alisema wako tayari kwa 'vita' ya kusaka ushindi na kila kitu ndani ya timu hiyo kimekaa vyema.

"Mechi itakuwa ngumu kwa sababu timu zote za Afrika Mashariki, na kocha wangu ametoka kwenye hii timu, hivyo yeye anaifahamu, lakini pia wachezaji watataka kumthibitishia pamoja na yeye kuondoka lakini wapo imara, tumejipanga vizuri kwa kuchukua pointi zote tatu. Tunakwenda kujikakamua ili kupata ushindi katika mechi hii," alisema Onyango.

Aliongeza kupoteza mechi dhidi y Horoya na Raja Casablanca kusiwafanye mashabiki kuvunjika moyo kwa sababu wachezaji wanaamini wanaweza kupindua meza.

"Baada ya matokeo yaliyopita wachezaji tumeambizana kuwa sasa ni mwisho kupoteza mechi, tunaenda kupambana kutafuta ushindi," Onyango aliongeza.

Mechi nyingine itakayochezwa leo ya kundi hilo itakuwa ni kati ya wenyeji, Raja Casablanca dhidi ya Horoya AC.

# Michezo

Jumamosi Februari 25, 2023

Nipashe




UKURASA 21

## Ten Hag awapigia saluti nyota United




Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' (kulia), akizungumza kuhusu maandalizi ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers FC itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa St. Mary's ulioko Entebbe, Uganda. Kushoto ni beki wa timu hiyo, Joash Onyango. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA, VIPERS VITA YA MAJIRANI

●●● Robertinho aahidi kuwashangaza Waganda na kurejesha matumaini ya...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

NENO ushindi ndio jambo pekee linalosubiriwa na wanachama na mashabiki wa Simba wakati timu yao itakapowavaa wenyeji, Vipers FC katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa St. Mary's, Entebbe.

Mechi hiyo ya raundi ya tatu ya Kundi C itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Simba inahitaji ushindi ili kurudisha matumaini ya kusonga mbele kutokana na kupoteza mechi zake mbili za awali, ilichapwa bao 1-0 ugenini Guinea dhidi ya Horoya AC halafu ikafungwa mabao 3-0 dhidi ya Waarabu wa Morocco, Raja Casablanca, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Endapo itapata ushindi, itarudi kwenye ushindani wa kuwania nafasi ya kusonga mbele na kurudia rekodi ya msimu uliopita ilipofika hatua ya robo fainali, iliondolewa na Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' amesema anafahamu mechi hiyo itakuwa ngumu si kwa sababu wao wanahitaji ushindi, lakini hakuna mechi nyepesi katika mashindano hayo ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Robertinho alisema wamekwenda Uganda kwa kazi moja ya kufuata pointi tatu ambazo wametumwa na wanachama, mashabiki wa Simba na nchi ya Tanzania kwa ujumla.

Mbrazil huyo alisema wamejiandaa kuwashangaza wengi katika mchezo huo muhimu kwa timu yake.

"Nafikiri itakuwa nzuri na ngumu, hakuna mechi yoyote ya Ligi ya Mabing-

INAENDELEA UK. 23

## Nabi : Tunaitaka robo fainali CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwasili salama nchini Mali na kukutana na hali ya joto kali, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema kazi kubwa aliyonayo ni kuwajenga kisaikolojia wachezaji kuelekea mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya AS Real de Bamako utakaochezwa kesho.

Yanga iliyofikia katika hoteli ya kifahari ya Granada-Lamitie iliyopo mjini Bamako, inahitaji ushindi ili kujiimarisha kwenye msimamo wa Kundi D kwa malengo ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Nabi aliliambia gazeti hili kikosi kiliwasili salama, wachezaji wote wapo katika hali nzuri lakini wamekutana na joto kali zaidi ya lililopo Dar es Salaam.

Kocha huyo alisema anaendelea kuwajenga wachezaji wake kuhakikisha wanakuwa makini na wanapambana kupata matokeo chanya.

"Nyuzi joto ipo juu sana, iko 38, hata joto la Dar es Salaam lina afadhari, kikubwa tunamshukuru Mungu tumefika salama, wachezaji wanatakiwa kuongeza umakini zaidi katika mechi ya Jumapili, tunajua itakuwa na ushindani mkubwa.Tunahitaji kufanya vizuri katika mchezo huo," alisema Nabi.

Aliongeza kikosi kitakachocheza mechi dhidi ya Real Bamako kitakuwa na kile kilichowapata ushindi dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

"Malengo yetu ni kutafuta pointi tatu muhimu ili kujihakikishia njia ya kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hii. Hatutaki kuondolewa mapema, uwezo na nia tunayo," Nabi alisema.

Katika msimamo wa Kundi D, Yanga iko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi tatu baada ya kupata ushindi wa mabao 3-1 kwenye mechi yake ya pili dhidi ya TP Mazembe.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara waliacha kwa kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa US Monastir ya Tunisia katika mechi ya kwanza iliyochezwa jijini, Tunis.

Mechi hiyo ya Real de Bamako dhidi ya Yanga itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania kwenye Uwanja wa Stade Modibo Keita.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >